SportPesa
TZS. 985,669,400
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**TAMISEMI** yataka ma-DED kumaliza kero matundu vyoo

UKURASA 4

Nipashe

Jumatano Machi 2, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580872

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



**LAPORTA: DEMBELE ATABAKI BARCELONA**

UKURASA 21

# Serikali ilivyoshtuka bei mpya ya mafuta

• **Kama** isingepunguza tozo ya 100/- ingekuwa maumivu, bei mpya zapanda kiduchu... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2
**KESI 50 UGAIDI, UHUJUMU ZAIVA**
MKURUGENZI wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu, amesema majalada...

UKURASA WA 3
**UJENZI WA SHULE YA MFANO WASUASUA**
NAIBU Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga...

UKURASA WA 5
**WAMWANGUKIA SAMIA MGOGORO ARDHI NA JWTZ**
WANANCHI wa Mtaa wa Kijaka Kimbiji, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni...

## Kisu, tofali vyatajwa kesi mauaji ya dada bilionea Msuya

UKURASA 3



Wafanyabiashara wadogo maarufu machinga wakiendelea na biashara zao kama kawaida kwenye mitaro ya maji ya mvua na njia za waenda kwa miguu, katika eneo la Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana, licha ya kuondolewa na serikali. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Watumishi watatu afya kortini madai ya rushwa

UKURASA 2

**MICHEZO** **HESABU ZA UBINGWA ZAMTESA NABI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Serikali ilivyoshtukia bei mpya ya mafuta

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

UAMUZI wa serikali kusitisha kwa muda tozo ya Sh. 100 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli nchini, utakuwa na ahueni kwa watumiaji wa nishati hiyo baada ya jana kutangazwa kwa bei mpya za bidhaa hizo zinazoanza kutumika leo.

Serikali kupitia Wizara ya Nishati juzi ilitangaza kusitisha kwa miezi mitatu kuanzia mwezi huu tozo ya Sh. 100 kwa kila lita ya petroli, dizeli na mafuta ya taa ili kukabiliana na kupaa kwa bei ya nishati hiyo, ambako huenda kungesababisha mfumuko wa bei ya bidhaa zingine.

Katika kile kinachoweza kutafsiriwa kama serikali 'ilishtuka mapema', jana kulitangazwa bei mpya za rejareja kwa bidhaa hiyo zitakazoanza kutumika leo, zikiongezeka kwa Sh. 60 na 65 kwa lita ya petroli na dizeli, mtawalia kulinganishwa na mwezi uliopita.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Ddooma, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Godfrey Chibulunje, alisema bei ya mafuta ya taa imepungua kwa Sh. 83 kwa lita.

Chibulunje alisema mabadiliko ya bei hizo yamechangiwa na kubadilika kwa bei za mafuta kwenye soko la dunia, gharama za usafirishaji na thamani ya Shilingi ya Tanzania kulinganisha na Dola ya Marekani.

"Bei hizi zingekuwa juu zaidi kama serikali isingechukua hatua ya kuahirisha tozo ya Sh. 100 kwa lita kwenye bei za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa," alisema.

Kiongozi huyo wa EWURA alibainisha kuwa bei za mafuta ya petroli na dizeli kwenye mikoa ya Kaskazini (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) zimeongezeka kwa Sh. 165 kwa lita.

Alitaja bei hizo kwa baadhi ya mikoa kuwa ni bei ya petroli kwa Dar es Salaam ni Sh. 2,540 kwa lita huku dizeli ikitakiwa kuuzwa kwa Sh. 2,403 na Sh. 2,208 kwa lita kwa mafuta ya taa.

"Kwa Arusha petroli kwa lita ni Sh. 2,620, dizeli (Sh. 2,541) na mafuta ya taa ni Sh. 2,292. Kwa Mkoa wa Dodoma petroli ni Sh. 2,599, dizeli ni Sh. 2,462 na Sh. 2,267 kwa lita ya mafuta ya taa," alisema.

Aliongeza kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya Mwaka 2015, kifungu namba 166, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko.

Alivitaka vituo vyote vya mafuta kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na kuonyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika.

"Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja, adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika," alisema.

Alisema wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za kielektroniki za pampu (EFPP) na wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo zinazoonyesha bei kwa lita.




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania, Manfredo Fanti (kulia kwake), alipofika Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Watumishi afya kortini kwa tuhuma za rushwa

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Kahama mkoani Shinyanga, imewafikisha mahakamani watumishi wa Kituo cha Afya cha Ukune kwa tuhuma za kuomba rushwa ya Sh. 14,500 kutoka kwa mgonjwa.

Watumishi hao ni Maneno Mbilikwa (29) na Elimekyus Leonard (31), ambao walifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kahama.

Wafanyakazi hao waliomba rushwa kutoka kwa Elizabert Jackson mkazi wa kata hiyo.

Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU wilayani Kahama, Simon Mashingiya, aliiambia mahakama kuwa tukio hilo lilitokea Desemba 7, 2021 katika Kituo cha Afya Ukune wakati mgonjwa huyo alipokwenda kupatiwa huduma za afya.

Mashingiya alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Donasian Augustine kuwa watumishi hao wameshtakiwa kutokana na kufanya kitendo hicho kinyume cha sheria.

Wakati huo huo Valence Ndagasu (33), mtumishi wa kitengo cha maabara katika Kituo cha Afya Ukune Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama, anatuhumiwa kujipatia Sh. 60,000 kutoka kwa Jumane Dotto kama rushwa kinyume cha sheria ili kumpatia damu.

Mwendesha mashtaka wa TAKUKURU, Simon Mashingiya, alidai kuwa tukio hilo lilitokea Desemba 7, 2021.

## Kesi 50 ugaidi, uhujumu zaiva

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu, amesema majalada takribani 50 kati ya 110 yamekamilika kupitiwa yakiwamo yahusuyo kesi za ugaidi, uhujumu uchumi na mauaji, na kwamba mashtaka yataanza kusikilizwa hivi karibuni.

Amesema majalada takribani 50 ya ugaidi, yamekamilika na kwamba baadhi yake baada ya kupitiwa na kukosa ushahidi yamefutwa, huku waliofutiwa mashtaka wakipewa sharti la kuripoti vituo vya polisi walioko.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, baada ya kuzindua mafunzo ya mfumo wa kielektroniki uitwao 'Case Management System, ambao utawezesha hati za mashtaka, kumbukumbu za kesi zinazosajiliwa polisi na kufikishwa mahakamani kuonekana papo hapo.

Mafunzo hayo ambayo yametolewa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Mawasiliano na yanatolewa kwa waendesha mashtaka mawakili na maofisa polisi kutoka mikoa yote nchini kwa awamu tofauti.

Akifafanua zaidi, DPP alisema majalada hayo yakiwamo yalikuwa ya mauaji mashtaka yake yameshushwa kuwa mauaji bila kukusudia, kutokana na mengi yake ushahidi wake kushuka.

"Majalada ambayo tumeyapitia kwenye ofisi yangu kwa miezi sita, ni yaliyokamilika yataanza kupelekea mahakamani hivi karibuni baada ya mahakama kupanga usikilizaji. Majalada haya mengine ambayo mfano yapo 10 utakuta nane ndio yana ushahidi," alisema Mwakitalu.

Akizungumza kuhusu mfumo huo ambao umeanza kutumika mkoani Mbeya, Mwanza na Arusha, DPP alisema sasa ofisi yake itaweza kufahamu majalada yaliyosajiliwa kila siku nchi nzima na kwamba itasaidia kuondoa mrundikano wa kesi.

Alisema kwamba changamoto kubwa iliyoko kwenye mahakama ni mrundikano wa kesi nyingi tangu mwaka 2000 kwa sababu ya kukosa upelelezi, alisema hivi sasa itakuwa rahisi kufahamu majalada yanayosajiliwa kila siku.

"Teknolojia inakua, hatunabudi kuwa na mfumo rafiki mahakamani. Kila mahakama, polisi itakuwa na kompyuta ingawaje si mara moja, ila zitakuwapo ili kufanikisha hili. Mfumo huu utaunganishwa polisi na mahakamani," alisema DPP.

Wakili wa Serikali Mwandamizi Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Dodoma, Beatrice Mpembo, alisema, mfumo huo utarahisisha majukumu yao na kwamba vitendea kazi vikiwapo kila mahali itasaidia jukumu hilo kufanyika kila mkoa.

Mkaguzi wa Polisi, Mwendesha Mashtaka, Wilaya ya Kilwa, Juma Ndaile, alisema hivi sasa majalada yatakuwa hayamalizi saa 48 bila kusajiliwa kwenye mfumo huo.

## Ujenzi wa shule ya mfano wasuasua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, ameonyesha kutoridhishwa na ujenzi wa shule ya mfano iliyoko eneo la Iyumbu jijini Dodoma kutokana na kutokamilika kwa wakati.

Mradi huo ulipaswa kukamilika Februari 22, mwaka huu, lakini mkandarasi wa ujenzi huo kutoka Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) ametaja sababu za kiufundi zilizosababisha mradi kushindwa kukamilika kwa wakati ikiwamo upatikanaji wa vifaa vya ujenzi, huku akiomba kupewa miezi sita ili akamilishe.

Akizungumza juzi alipotembelea na kukagua ujenzi huo, Kipanga alisema: "Mimi sijaridhishwa kwa sababu mradi ulipaswa kukamilika Februari 22, mwaka huu, lakini imefika mradi haujakamilika tafsiri yake yale malengo tuliyojiwekea hatujafikia."

Alisema kwa sasa ilitakiwa kufanyika makabidhiano ya mradi, lakini mpaka sasa ujenzi wake umefikia asilimia 62 na mkandarasi anaomba kuongezwa muda.

"Bila kupepesa macho ndugu zangu hatujaridhishwa, tunaenda kufanyia kazi... niahidi hapa mbele yenu changamoto zote ambazo zimesababisha kuchelewa kwa mradi huu tutazifanyia kazi.

"Ijumaa (Machi 4, 2022) tutakuwa na kikao cha kuzijadili changamoto zote ambazo zimesababisha mradi kuchelewa," alisema.

Aliongeza kuwa wizara itaangalia muda wa kuongezwa baada ya kupitia sababu za mkandarasi ili ifikapo Juni mwaka huu wanafunzi wa kidato cha tano watakaochaguliwa waanze kutumia majengo hayo.

Alibainisha kuwa mradi huo unagharimu Sh. bilioni 17.1 ambayo itakuwa shule ya mfano nchini na itakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita 1,000 wa kike na kiume.

"Kuna changamoto za kiufundi nimeziona. Kwa kuwa tutakaa kwenye kikao cha kitaalamu, nitazieleza huko ili kurekebisha upungufu uliojitokeza," alisema.

Naibu waziri huyo alisema serikali imeendelea na dhamira yake ya kujenga shule 1,000 nchini ambapo tayari fedha zimetolewa na kwa mwaka wa fedha 2021/22, zaidi ya shule 274 zikiwa kwenye mchakato wa ujenzi. "Vilevile, serikali ilikusudia kujenga shule 26 za sayansi za wasichana na tayari ujenzi umeanza kwenye mikoa 10 na unaendelea, nimpongeze Rais kwa kazi kubwa anayofanya," alisema.

# Kisu, tofali, kitambaa vyadaiwa kutumika mauaji dada wa Msuya

**KULWA MZEE**

KISU, tofali na kitambaa vimedaiwa kuwa vilitumika katika mauaji ya aliyekuwa dada wa Bilionea Msuya, Aneth Msuya, Kibada, Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

Madai hayo yalitolewa jana na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Mrakibu Mwandamizi (SSP) Richard Mwaisemba (48) wakati akitoa ushahidi wake katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam mbele ya Jaji Ediwin kakolaki.

SSP Mwaisemba ni shahidi wa nne katika kesi hiyo ya mauaji inayomkabili Miriam Mrita ambaye ni mjane wa marehemu Bilionea Msuya na mwenzake.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Genes Tesha, alidai kuwa Mei 26, 2016 akiwa Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Kigamboni, alipata taarifa kwamba kuna mauaji ya mwanamke Block 17 Kibada, Kigamboni.

Alidai kuwa alichukua askari saba na kwenda eneo la tukio na walipofika walikuta watu wengi, akiwamo mwenyekiti wa eneo hilo. Alidai kuwa aliiongozwa na mwenyekiti na kuingia katika chumba alichokuwa Aneth.

"Chumbani nilikuta mwili wa mwanamke umelala chini ukiwa hauna nguo, damu imetapakaa chini, kichwa kiliangalia dirishani, miguu ilielekea mlangoni.

"Nilipoangalia pembeni kulikuwa na nguo ya ndani na katika sofa chini kulikuwa na kisu. Wakati tunatoka mlango wa kuingia chumbani ulionekana ulikuwa haujafungwa na funguo, uligongwa na tofali ukafunguka," alidai.

"Mlango wa kuingia katika nyumba hiyo unaonekana ulifungwa kwa funguo, uligongwa na tofali ukafunguka na kupasuka ubao. Chini vipande vya tofali na mchanga vilikuwapo," aliongeza kudai SSP Mwaisemba.

Alidai kuwa baada ya kuona vitu hivyo, alimpigia Mkuu wa Upelelezi Mkoa ili apeleke timu ya wataalamu wa uchunguzi na kuchukua vielelezo.

Mwaisemba alidai kuwa wataalamu walifika na kufanya uchunguzi na walipomaliza, yeye na askari wake walichukua mwili na kuupeleka kuhifadhi Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Shahidi wa tatu, Mwanaisha Kassim, anayeishi jirani na nyumba ya marehemu Aneth Msuya, alidai kuwa anakumbuka akiwa nyumbani kwao, saa mbili asubuhi, alifuatwa na Allan wakati huo akiwa na miaka minne na kumwambia hamwoni mama yake, aitwaye Aneth.

Mwanaisha alidai kuwa aliongozana na Allan pamoja na Swaumu Ramadhan hadi nyumbani kwa Anneth, walikuta geti na mlango wa jikoni uko wazi, alibisha hodi lakini hakuitikiwa.

"Allan aliniingiza chumbani, akasema njoo umwone mama yangu kalala. Nilipoingia nilikuta mama yake kalala chini chali, hana nguo kafunikwa kitambaa usoni, chini damu ilitapakaa ikitokea shingoni.

"Nilishtuka nikatoka nje. Niliomba msaada kwa mama ntilie. Walipokuja kuona niliondoka, sikujua nini kiliendelea," alidai Mwanaisha. Akihojiwa na Wakili Peter Kibatala, alidai katika maelezo yake ya onyo kwamba Aneth alikuwa amelala chali, akiwa amefunikwa kitambaa usoni na sehemu za siri na msichana wake wa kazi hakuwamo ndani ya nyumba hiyo.

Mwanaisha alidai kuwa askari alimfuata nyumbani kuchukua maelezo yake na chumba ambacho mwili aliukuta, hakukuta viashiria vya kuonyesha kuwa ni chumba cha watoto.

Pia alidai kwamba hakuona chupi, filimbi wala kisu chumbani isipokuwa mlangoni aliona vipande vya matofali.

Washtakiwa katika kesi hiyo ya mauaji ni mke wa marehemu bilionea Erasto Msuya, Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyella.

# NOTISI/TANGAZO

MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MBAGALA | OSCAR ELIAMINI CHUWA | NYUMBA | FLORA ELIAMINI CHUWA | MBAGALA KIZUIANI | 16/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | NASHON RANGE ROTENTE | NYUMBA NA KIWANJA | NASHON RANGE ROTENTE | NYUMBA- MBONDOLE NA KIWANJA- PUGU | 17/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | MBOPO HARDWARE AND TOFALI INVESTMENT | NYUMBA | MBOPO HARDWARE AND TOFALI INVESTMENT | MBOPO | 18/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | PAULO GIREMBE RAWE | NYUMBA | PAULO GIREMBE RAWE | KIVULE | 16/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | AMEDEUS ALFONCE KIMATH | NYUMBA | BEATRICE GELAZI MTAKYAWA | MBEZI-KWAMSUGULI | 21/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | DENIS JEREMIAS KIVIKE | NYUMBA | DENIS JEREMIAS KIVIKE | CHANIKA | 22/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | OBEDI ZIHIRWADI MSINGA | NYUMBA | OBEDI ZIHIRWANI | KONGOWE-KIBAHA | 22/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | EVALYNE PAULO SAITERU | NYUMBA | EVALYNE PAULO SAITERU | BONYOKWA | 17/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | HIZA SHABANI MTIPA | NYUMBA | HIZA SHABANI MTIPA | KISEMVULE | 18/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | BOSCO THADEI UTENGA | NYUMBA | BOSCO THADEI UTENGA | KIGEZI JUU | 16/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | ISMAIL ISSA MICHAEL | NYUMBA | ISMAIL ISSA KASANGA | CHANIKA LUBAKAYA | 16/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | SEVERINI BONAVENTURA LYIMO | NYUMBA | SEVERINI BONAVENTURA LYIMO | MTONGANI-KUNDUCHI | 17/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | JACKLINE KANTE WILLIUM | NYUMBA | NICHOLAUS DAVID LYANGA | KEREGE-BAGAMOYO | 18/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | ELISANTE BERNADI MRTA | NYUMBA | ELISANTE BERNAD MRTA | SOMANGILA-KIGAMBONI | 22/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | KIPEJA TIMBER AND GENERAL SUPPLIES | NYUMBA | JOHN TIMOTH PANGANI | IGOMA-MWANZA | 17/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | STEVEN PIUS MALISA | NYUMBA | STEVEN PIUS MALISA | MTAA WA KIPUNGUNI 'B'-KITUNDA | 22/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | BUMERA LODGE AND CO. LTD | NYUMBA | JOACHIM HERONIMUS MWINGIRA | MTAA WA KIGOGO KATI | 21/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | DIANA JUDICATE PETER | GARI TOYOTA PORTE NO.T786 CVZ | DIANA JUDICATE NDENGERIO | CHANG'OMBE TEMEKE | 18/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |

| | MASHARTI YA MNADA |
|---|---|
| 1 | Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba ,Kiwanja au Gari ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14. |
| 2 | Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolote la mnada kuhusiana na malipo yaawali,hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa. |
| 3 | Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0784252048/0713077474/0718038313/0714939933/0754497396/0768672367 |
| 4 | Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote. |

# TAMISEMI yataka wakurugenzi kumaliza kero matundu ya vyoo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amewataka wakurugenzi wa halmashauri kutumia bajeti zao za mwaka 2022/2023 kumaliza kero ya upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini badala ya kuendelea kumtegemea Rais kwa kila kitu.

Bashungwa, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), katika mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema, badala ya kuendelea kumtegemea Rais Samia kwa kila kitu, wakurugenzi wanatakiwa kuwa wabunifu ili kumaliza kero hiyo ya upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini.

"Kero ya matundu ya vyoo katika shule za sekondari na msingi lazima wakurugenzi tujiongeze, Rais ametupa madarasa tena na vyoo, nataka bajeti ya mwaka huu hili jambo liwe kipaumbele kwenu kila mmoja ahakikishe linakwisha kwani hadi sasa tuna upungufu wa matundu ya vyoo 295,072 kwa shule za msingi na sekondari matundu 44,603," alisisitiza Bashungwa.

Aliwataka watumishi wote katika mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha fedha zote ambazo zimetolewa na Rais zinatumika kama ilivyokusudiwa na siyo vinginevyo.

"Serikali ya awamu sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, imetoa fedha nyingi sana kwenda katika halmashauri nchini hivyo mnao wajibu wa kwenda kuzilinda kwa uadilifu na atakaye kwenda kinyume hatuta mfumbia macho," alisema Bashungwa.

Kadhalika, alisema katika kipindi cha miezi 11 kuelekea mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia, wizara yake imepokea jumla ya Sh. trioni 1.49 ambazo zimekwenda katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 662.32 zimekwenda katika sekta ya elimu na zimetumika katika ujenzi wa vyumba vya madarasa 4,525, nyumba za walimu 42 matundu ya vyoo 568, vyumba vya maabara 11, mabweni 170, mabwalo sita, majengo ya utawala manne katika shule za msingi na sekondari.

"Na katika kipindi cha kuanzia mwezi Machi hadi Julai mwaka huu, kiasi kingine cha Sh. bilioni 72.96 kinakwenda kutolewa ili kazi iendelee katika sekta ya elimu," alisema. "Kupitia fedha hizi tunatarajia kujenga vyumba vya madarasa 300, kwa ajili ya wanafunzi wa darasa la awali, madarasa 3,468 kwa shule za msingi na sekondari, mabweni 221, mabweni 20 kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum pamoja na ukarabati wa vituo vya walimu," alisema.

Katika sekta ya afya alisema wamepokea Sh. bilioni 234.1 ambazo zimetumika katika ujenzi wa vituo vya afya 288, hospitali mpya za wilaya 28, zahanati 615, hospitali 68.

"Na katika kipindi cha Machi hadi Julai 2022, tunatarajia kupokea Sh. bilioni 263.72 zitakazo tumika katika ujenzi wa vituo vya afya 288, hospitali 28, zahanati 167 kukamilisha ujenzi wa hospitali 68 za wilaya zilizoanza kujengwa katika mwaka wa fedha 2018/19 kuendeleza hospitali 37 za halmashauri pamoja na ununuzi wa vifaa vya huduma za wagonjwa mahututi, magari ya kubeba wagonjwa 195," alisema.

Katika sekta ya barabara alisema kupitia Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA), wamepokea Sh. bilioni 597.

Alisema katika kiasi hicho cha fedha wamejenga barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilomita 213 na changarawe kilomita 1,152.

"Tumefanya matengenezo ya barabara kilomita 25,059, ujenzi wa madaraja 201 ambapo ujenzi unaendelea, tumejenga box karavati 70 pamoja na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita 125," alisema Bashungwa.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema utaratibu wa wizara kutoa mafanikio katika kipindi cha mwaka mmoja wa serikali ya awamu ya sita utahusisha wizara zote.

"Leo mheshimiwa Bashungwa tumeanza na wewe ambaye umetufungulia hili, lakini wizara zote zitashiriki kueleza mafanikio yao kuanzia leo hadi Machi 16, mwaka huu na nitoe rai kwa wahusika kila mmoja kuhakikisha kuwa anashiriki kueleza umma mambo mazuri yaliyofanyika na serikali ya mama Samia," alisema Msigwa.



Vijana wanaoishi katika mazingira magumu kutoka kata tatu za Wilaya ya Mufindi, mkoa wa Iringa, wakiwasilisha malengo yao wakati wa warsha ya afya ya akili inayoendeshwa na mradi wa Youth Agency Mufindi, jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## 'Wanawake wa Kiafrika msingi wa ajenda AfCFTA'

**Na Jenifer Gilla**

WANAWAKE wa Kiafrika wametambuliwa kama wahusika wakuu katika utekelezaji wa soko huria katika Bara la Afrika (AfCFTA) kwenye mdahalo wa pembeni uliofanyika Februari 28, mwaka huu, ikiwa ni maandalizi ya kikao cha nane cha Jukwaa la Kanda ya Afrika la Maendeleo Endelevu (ARFSD), utakaofanyika kuanzia Machi 3 hadi 5, 2022 mjini Kigali nchini Rwanda.

Naibu Katibu Mtendaji wa Tume ya Uchumi Afrika (ECA's), Antonio Pedro, alieleza katika mkutano huo kwamba AfCFTA inategemea uwekezaji katika usawa wa kijinsia na kusisitiza umuhimu wa kukabiliana na vikwazo ambavyo wanawake wanakumbana navyo katika kushiriki kwenye uchumi ili kupunguza ukosefu wa usawa kati ya wanaume na wanawake.

Kikao hicho ambacho kiliangazia umuhimu wa AfCFTA katika kufikia usawa wa kijinsia kufikia Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDG 5) na Agenda 2063 barani Afrika pia kilijadili changamoto na matarajio ya kutumia fursa zinazotolewa na biashara na AfCFTA kuelekea usawa wa kijinsia.

Kikao hicho pia kilitoa mwanga kuhusu umuhimu wa sera na sheria zinazozingatia jinsia ili kuweka mazingira wezeshi ya kutekeleza AfCFTA kwa mafanikio na kutimiza matarajio ya Ajenda 2063.

Mama Keita, Mkurugenzi wa Ofisi Ndogo ya Kanda ya Tume ya Uchumi Afrika (ECA) ya Afrika Mashariki, alibainisha kuwa biashara zinazomilikiwa na wanawake barani Afrika zinachangia asilimia 60 ya pato la taifa. Wanawake wanaweza kushiriki kikamilifu katika biashara ikiwa wanaishi maisha ya kujitawala.

"Ni jukumu letu kuondoa vikwazo katika maendeleo ya bara, kutoa fursa na kupima mafanikio kupitia macho ya wanawake na vijana," alisema.

Wakati Waziri wa Jinsia na Ukuzaji wa Familia wa Rwanda, Jeanette Bayisenge, alieleza kuwa ingawa nchi yake imepata mafanikio makubwa katika haki za wanawake, bado kuna changamoto nyingi.

"Kwa hivyo AfCFTA, ina uwezo mkubwa wa kuwa suluhu kupitia utekelezaji unaozingatia jinsia," alisema.

Hafla hiyo ilifanyika kuelekea mkutano wa nane wa Jukwaa la Kanda ya Afrika la Maendeleo Endelevu (ARFSD), kilichoandaliwa na Tume ya Uchumi Afrika (ECA) na Serikali ya Rwanda kwa ushirikiano na Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Benki ya Maendeleo ya Afrika na mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa. Mkutano huo unaongozwa na kaulimbiu "Kujenga mbele bora: Afrika ya kijani, jumuishi na yenye uthabiti iliyo tayari kufikia Ajenda ya mwaka 2030 na ile ya 2063."

# Waziri awafunda wanaoishi na VVU Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU wanaoishi na virusi vya UKIMWI (VVU) mkoani Njombe, wametakiwa kujitokeza na kuunda vikundi ambavyo vitawawezesha kupata mikopo kwa ajili ya kufanya shughuli za ujasiriamali.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge, Pindi Chana, alisema hayo jana baada ya kutembelea vikundi vya ujasiriamali kwa watu wanaoishi na VVU katika Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Alisema serikali iko tayari kutoa uwezeshaji wa elimu pamoja na mitaji kwa wale watakaokuwa tayari kuunda vikundi vya ujasiriamali.

Waziri alisema watu wakiunda vikundi na kushiriki shughuli za ujasiriamali, watapata fursa ya kusomesha watoto wao kwa kuwa serikali tayari imeshajenga madarasa ya kutosha.

Alisema ameamua kutembelea vikundi vya ujasiriamali kwa watu wanaoishi na VVU kuanzia kwenye mashamba yao hadi bidhaa wanazotengeneza ili kujionea shughuli zinazofanywa na vikundi hivyo. "Kwa hiyo ndugu zangu tujitokeze tusibaki nyuma, tuchape kazi kwani serikali iliyopo madarakani inawapenda," alisema.

Pindi alilipongeza Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI Tanzania (NACOPHA) kwa muundo wao mzuri kuanzia ngazi ya taifa mpaka vijiji.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI Tanzania, Joselyn Mtono, alisema watu hao ukimwi wanatakiwa kuwa wawazi na kujiunga na konga ili kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo.

Aliwataka kuacha kujinyanyapaa na kujitenga ili ifikapo mwaka 2030 kusiwe na maambukizi mapya ya VVU au kutokomeza kabisa ugonjwa huo.

"Hali ya kuishi na VVU si tatizo ambalo linaweza kumfanya mtu kushindwa kufanya shughuli zozote za maendeleo bali wanaweza kufanya na kumudu maisha yao," alisema Mtono.

Alilishukuru Shirika la Misaada ya Maendeleo la Marekani (USAID) kwa kuwawezesha kutembelea vikundi hivyo vya watu wanaoishi na VVU katika Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, alisema miaka ya nyuma, tume hiyo ilikuwa na miradi ya kuwasaidia watu wanaoishi na VVU kwa kuwapatia fedha za kujikimu kimaisha lakini kwa sasa kuna changamoto ya upatikanaji wa fedha.

Dk. Maboko alisema kitendo cha vikundi hivyo vya watu wanaoishi na VVU kushiriki katika shughuli za maendeleo kabla ya serikali kuunga mkono jitihada zao, ni jambo la faraja.

"Huko nyuma sana TACAIDS tulikuwa na miradi ya kuwasaidia watu wanaoishi na VVU. Tume ilikuwa inaleta fedha kwa ajili ya kujikimu kimaisha, lishe na miradi mbalimbali," alisema Dk. Maboko.

Baadhi ya viongozi wa vikundi vya watu wanaoishi na VVU kutoka kikundi cha JIUKU, Rajabu Mligo, na kikundi cha FAKISHU, Grace Kabindu, walisema kuishi na maambukizi ya VVU si sababu ya kushindwa kufanya shughuli za maendeleo.

"Sisi kama wanakikundi tumepata mafanikio makubwa kutokana na shughuli zetu za ujasiriamali kwani tumejenga pamoja na kusomesha watoto wetu," alisema.

HABARI KITAIFA

## Balozi Ujerumani, Bashe kujadili anuwai za vyakula vya Kitanzania

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

BALOZI wa Ujerumani nchini, Regine Hess, na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, wanatarajiwa kuwaongoza zaidi ya watu 3,000 kutoka Tanzania na nchi jirani za Afrika Mashariki, kuona na kujivunia anuwai za vyakula vya kitanzania. Zaidi ya kampuni 120 za ndani na nje ya nchi zitashiriki kwa pamoja kuona na kujivunia kile kinachoitwa 'ladha ya Tanzania' hasa sekta ya kilimo inavyochangia kuajiri na kutoa mchango mkubwa kwa pato ghafi la taifa.

Jana, Mkurugenzi Mwenza wa Kampuni ya KILIFAIR Promotion Ltd, inayoandaa maonyesho ya biashara ya kimataifa, Dominick Shoo, alisema Balozi Hess na Bashe, Machi 11, mwaka huu, watazindua maonyesho hayo maarufu kama TANZFOOD Expo 2022 yatakayofanyika jijini hapa.

"Tunaelewa kwamba sekta hii si tu kwa ajili ya taifa letu la Tanzania, bali inalisha nchi zingine nyingi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hii ndiyo sababu tuliamua kuwekeza katika maonyesho yenye viwango vya kimataifa ili kwamba tujivunie vya kutosha na kuonyesha ladha ya Tanzania kama kibwagizo cha maonyesho hayo kinavyosema.

"Na sisi tunafurahi kuona mwitikio wa waonyeshaji kutoka ndani ya Tanzania na masoko mengine. Maonyesho haya si tu yanaonyesha bidhaa, bali itawaleta wataalamu mbalimbali wa sekta ya kilimo ili kutoa ujuzi wao kikamilifu kwa kampuni zinazoshiriki na wakulima watakaofika katika maonyesho hayo yatakayofanyika viwanja Magereza, Arusha kuanzia Machi 11 hadi 13, mwaka huu," alisema. Kwa mujibu wa Shoo, tayari waandaaji wa maonyesho hayo wameanzisha semina na warsha ili kuwaelimisha wakulima kuhusu kuongeza ubora na maendeleo katika sekta ya kilimo.

"Wageni watatumia maonyesho hayo kujenga mtandao wa kibiashara katika mazingira rafiki ya kitaalam na anuwai za vyakula vya kitanzania.

Aidha, Meneja Mkuu wa Maendeleo wa Asasi Kilele inayojishughulisha na kilimo cha maua, mboga, matunda, viungo na mazao yatokanayo na mizizi (TAHA), Anthony Chamanga alisema: "Sisi tuna wakulima 19,700 ambao wanazalisha bidhaa za mboga zenye ubora wa juu zinazokidhi viwango vya masoko ya kimataifa.

"Kwa hiyo tunafurahi kwamba wanachama wetu wataona fursa tele zilizoko katika sekta ya kilimo na jinsi gani ushiriki wao katika sekta hii unavyoweza kusaidia kupeperusha bendera ya taifa katika masoko ya kimataifa."

Naibu Meneja Mipango wa Shirika la Miradi la Ujerumani (GIZ), Bernd Schmidt, alisema anaamini maonyesho hayo, licha ya kuwaletaa pamoja wakulima na wafanyabiashara kutoka kampuni za ndani na nje ya nchi zinazohusiana na kilimo, Tanzania itanufaika kupata ujuzi na ubunifu katika kilimo, ufungashaji, usindikaji, mbegu bora, pembejeo za kilimo, viuatilifu na kemikali.

Naye Mkurugenzi wa Sekta ya Uzalishaji wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Jean Baptiste Havugimana, alisema EAC imewekeza kiasi kikubwa katika kuwajengea uwezo wakulima wa Tanzania na wadau wengine wa kilimo, kwa kuwapatia fursa rahisi katika sekta hiyo, hasa upatikanaji wa fedha zinazohitajika kuwawezesha kunufaika na rasilimali za kilimo.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (kulia), akizungumza na wakazi wa Kata ya Kipunguni, jijini Dar es Salaam jana, alipotembelea Taasisi ya Sauti ya Jamii Kipunguni, akiwa katika ziara ya kuimarisha Kamati za Kupinga Ukatili Ngazi ya Jamii (MTAKUWWA), wilayani Ilala. Kulia kwake ni Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ngh'wilabuzu Ludigija na Mwenyekiti wa Taasisi ya Sauti ya Jamii Kipunguni, Fatma Talib. **PICHA: SABATO KASIKA.**

# Watuhumiwa wa ugaidi waachiwa huru kortini

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imewaachia kwa masharti watuhumiwa 12 waliokuwa wakishtakiwa kujihusisha na vitendo vya ugaidi.

Washtakiwa hao waliokuwa wakishtakiwa kwenye kesi tano tofauti, waliachiwa jana kwa mahakimu tofauti baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuwasilisha hati akionyesha Jamhuri haina nia ya kuendelea na mashauri hayo.

Washtakiwa walioachiwa ni Hassan Mnele, Ramia Salehe, Juma Ally, Abdallah Omary na Nassoro Omary ambao walifikishwa mahakamani huko mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Yusto Ruboroga.

Washtakiwa wengine ni Juma Athuman na Ally Nassoro waliokuwa wamefikishwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Mbele ya Hakimu Evodia Kyaruzi, washtakiwa walioachiwa ni Seif Mwishehe, Yusuph Rajabu, Buheti Buheti, Hussein Juma na Haruna Nkuye.

Katika hatua hiyo, upande wa mashtaka uliowakilishwa na jopo la Mawakili wa Serikali Waandamizi, Waziri Magumbo na Ramadhan Kalinga na Wakili wa Serikali, Ashura Mnzava na Yusuph Aboudi, ulidai DPP hana nia ya kuendelea na kesi dhidi ya washtakiwa chini ya kifungu cha 91 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA).

Baada ya kueleza hayo, mahakimu wote waliwaachia huru washtakiwa wote na kusikiliza maombi ya upande wa mashtaka waliotaka washtakiwa wapewe masharti.

Upande wa mashtaka uliambatanisha maombi hayo chini ya kifungu cha 73, kifungu kidogo cha E, kifungu cha 74, 392 A na kifungu cha 2 cha CPA namba 20 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Walidai kuwa maombi hayo yameambatanishwa na kiapo cha SSP Jumanne Amos ambaye ni Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Kipolisi Temeke na kiapo cha SP Boniphace Mwakalegesye ili kuwa sehemu ya mwenendo wa kesi hizo.

Jamhuri iliomba mahakama hiyo iwaamrishe washtakiwa kuleta mahakamani wadhamini kwa lengo la kuthibitisha kuwa washtakiwa watakuwa kwenye uangalizi na kuangalia mwenendo wao wa kitabia kwa miaka mitatu. Pia waliomba washtakiwa wawe wanaripoti Kituo cha Polisi Temeke na Ilala mara mbili kwa mwezi kwa lengo la kufuatilia tabia zao na kwamba wasionekane wakitenda makosa ya jinai kwa miaka mitatu na mahakama ifikirie kutoa amri nyingine kwa kadri itakavyoona inafaa.

Baada ya kusomwa maombi hayo, washtakiwa wote walikubaliana na maombi hayo.

Hakimu Ruboroga aliwataka washtakiwa Mnele na Salehe kuripoti Kituo cha Polisi Temeke mara mbili kwa mwezi ndani ya miaka mitatu ili kuangalia mwenendo wa tabia zao.

Pia aliwataka kuwa na wadhamini wawili watakaotia saini dhamana ya maandishi ya Sh. milioni tano kila mmoja na kutotenda makosa ya jinai kwa kipindi cha miaka mitatu.

Washtakiwa Ally, Omari na Amiri wametakiwa kuripoti Kituo cha Polisi Ilala mara moja kwa mwezi ndani ya miaka mitatu kutokana na washtakiwa hao wawili ambao ni Omari na Amiri kuwa wakazi wa Zanzibar.

Hakimu Shaidi aliwataka washtakiwa kuwa na tabia njema wawapo nje sambamba na kuwa na wadhamini wawili watakaosaini dhamana ya Sh. milioni sita.

Hakimu Shaidi alisema utawala utashughulikia suala la kuripoti polisi baada ya washtakiwa kuomba mahakama iamuru waripoti mara moja na ikibidi vituo vilivyoko karibu nao.

Washtakiwa hao walidai walipokamatwa walikuwa wamepanga, hivyo hawajui kama wataendelea kuishi katika nyumba za awali au la.

Mbele ya Hakimu Kyaruzi, alisema masharti yaliyotolewa na mahakama yanazingatia mazingira yaliyopo hivyo aliwataka kila mshtakiwa awe na wadhamini wawili watakaosaini dhamana ya Sh. milioni tano na kuripoti polisi mara mbili kwa mwezi ndani ya miaka mitatu.

Inadaiwa sababu za kuleta maombi hayo ni washtakiwa Salim na wenzake walifunguliwa jalada la uchunguzi lenye namba C/IR/8993/2016 wakijihusisha na kosa la kula njama na vitendo vya kigaidi lililofunguliwa Mkoa wa Kipolisi Temeke.

Alidai washtakiwa walikamatwa Desemba 23, 2015 mpaka wa Manyovu mkoani Kigoma wakijaribu kuvuka mpaka kwenda nchi nyingine bila kuwa na nyaraka halali za kuvuka mpaka.

Washtakiwa hao walikuwa wakazi wa Temeke na walikuwa wanatafutwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma hizo.

Walikamatwa mkoani Kigoma na kurudishwa Dar es Salaam ambako taratibu za kuwafungulia kesi zilianza na uchunguzi uliendelea lakini Mkuu wa Upelelezi Temeke, SSP Jumanne baada ya kuchunguza tuhuma dhidi yao hawakuona nia ya kuendelea kuwashtaki. Alidai washtakiwa wakiachiwa bila masharti, wanaweza kuhatarisha maisha ya watu na usalama wa nchi kwa ujumla, hivyo waliona washtakiwa wapewe masharti endapo watakuwa nje.

Washtakiwa waliomba mahakama iwapunguzie masharti kwa kuwa kukaa gerezani tangu 2016, wamejifunza kuwa na tabia njema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali ifuatilie kwa karibu mafanikio kuondolewa tozo

**JUMATATU** serikali ilitangaza kuondoa tozo ya Sh. 100 kwa kila lita ya mafuta ya petroli, dizeli na ya taa kwa watumiaji kwa miezi mitatu kuanzia Machi hadi Mei mwaka huu, ili kupunguza mzigo na kuwarahisishia wananchi maisha.

Aidha, Waziri wa Nishati, Januari Makamba, alisaini kuridhia mabadiliko ya kanuni, huku utekelezaji rasmi wa mabadiliko hayo ukianza leo.

Uamuzi huo utaikosesha serikali mapato ya Sh. bilioni 30 kila mwezi, lakini lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi hawapati shida hasa katika kipindi hiki ambacho kuna vita ya Ukrein na Urusi, ambayo tayari imesababisha bei ya mafuta ulimwenguni kuongezeka.

Tunaipongeza serikali kwa uamuzi huu ambao ni muhimu kwa manufaa ya wananchi wa kawaida, matarajio ya wengi ni kuwa bei za bidhaa mbalimbali zitashuka kwa kuwa mafuta yameshuka.

Kupanda kwa bei ya mafuta kuna athari kubwa kwa bidhaa mbalimbali ambazo zinagusa maisha ya mwananchi moja kwa moja, inapotokea bidhaa zimeshuka faida siyo kwa waendesha magari pekee bali kwa wananchi wa kawaida.

Mfano anayeuza bidhaa za vyakula anasafirisha kwa gari kutoka shambani hadi sokoni, inapotokea bei ya mafuta imepanda bei ya kusafirisha huongezeka maana yake inabidi muuzaji wa bidhaa aongeze bei, ili faida yake iendelee kupatikana.

Tunaamini bei za mafuta kuanzia leo zimeshuka, ili mwananchi wa kawaida kabisa anufaike ni muhimu sasa serikali kufuatilia bei ya bidhaa mbalimbali.

Tunatambua kuwa biashara ni huria na serikali haipangi bei ya bidhaa lakini inasimamia kuhakikisha wananchi hawaumizwi sana, na katika kuona hali hiyo imeamua kuondoa tozo ili kusaidia zaidi.

Ili mwananchi wa kawaida aone ahueni iliyolengwa na serikali ni lazima bei za bidhaa zishuke, isipokuwa hivyo itakuwa hakuna tofauti kwake, kwa kuwa maisha ni yale yale.

Kama alikuwa ananunua mkate mkubwa Sh. 3,000 sasa bei irudi Sh. 2,500 ya awali, kwa kuwa sasa zimepanda kwa madai kuwa mafuta yamezidi kupaa, hali inayofanya maisha kuwa magumu na wengi kushindwa kumudu gharama za maisha.

Itapendeza kama baada ya miezi mitatu serikali itafanya tathmini kuona ahueni kwenye maisha ya kila na kuendelea kuondoa tozo hiyo, ili maisha yawe rahisi zaidi.

Tunatambua kuwa fedha hii iliongezwa kwa ajili ya Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA), ambaye anawajibu wa kusimamia barabara hizo.

Kwenye kila mkutano wa bunge, wabunge wengi wanapaza sauti juu ya hali mbaya ya barabara kila mmoja akieleza ni muhimu kwa maendeleo ya maeneo husika, huku madaraja na makalavati yakiharibika kiasi cha kukatisha mawasiliano baina ya eneo moja na jingine.

Kwa mabadiliko haya maana yake fedha hizo hazitapatikana, lakini tunaamini serikali imejipanga vyema hasa kutumia fedha za mikopo mbalimbali ambayo nchi imekuwa ikipata kwa ajili ya sekta mbalimbali ikiwamo miundombinu.

Tunaamini kwamba kutakuwa na ufuatiliaji wa karibu ikiwamo utekelezaji wa maelekezo ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji juu ya kupanda kwa bidhaa za vyakula na ujenzi ambako kumelalamikiwa na wananchi kwa muda mrefu.

Ni muhimu kufanya hivyo kwa kuwa baadhi ya wafanyabiashara wasiowaaminifu hupandisha bei kwa lengo la kujipatia faida kubwa, huku wananchi wakiumia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Rais Samia kiongozi mtumishi, karata ya kujivunia kinamama

Na Reubeni Lumbagala

**KUANZIA** jana dunia inatazama kazi nyingi za wanawake. Kuelekea kilele cha Siku ya Kinamama Duniani Machi 8. Maadhimisho hayo yanafanyika kila mmoja akimtazama mwanamama ambaye ni mwanajamii, mlezi, mzazi na kiongozi wa familia ambaye kila mmoja atakubali kuwa ni nani kama mama.

Wanawake wa Tanzania nyuma ya Rais Mama Samia Suluhu Hassan, wamedhihirisha kuwa kinamama ni viongozi bora na hilo linabainishwa na vigezo vingi alivyo navyo Rais.

Sifa mojawapo ya kuwa kiongozi ni kuwa mtumishi mwenye msukumo wa kuwatumikia wale unaowaongoza ili kufikia ustawi bora kwa maendeleo.

Nguzo kuu ya kiongozi mtumishi inayoonekana kwa Rais Samia ni kuwatumikia wengine na kutanguliza maslahi yao.

Jambo zuri zaidi kuhusu Rais ni kuwajibika ipasavyo katika majukumu yake ili kufikia dira na malengo waliyojiwekea Watanzania.

Uwajibikaji kwa kiongozi mtumishi kama Rais Samia si hisani bali wajibu wa msingi katika kusaidia kufikia kwa maendeleo ya wananchi.

Kimsingi, taasisi, jamii au nchi zinazoongozwa na viongozi watumishi kama alivyo Rais hufanikiwa kwa haraka katika kupiga hatua za kimaendeleo katika nyanja zote yaani kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Hii ni kutokana na ukweli kuwa viongozi watumishi huzingatia kuwa nafasi walizonazo ni dhamana kwa ajili ya kuwatumikia watu na si kutumikiwa kama baadhi ya viongozi wanavyofanya kwa baadhi ya mataifa.

Kiongozi mtumishi anatenga muda wa kusikiliza kero za wananchi ili kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu. Rais Samia aliweka bayana msimamo wake mapema kwa wateule na wasaidizi wake kuhakikisha wanatenga siku maalum za kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi. Alisisitiza kuwa katika ziara zake akikutana na mabango ya wananchi yenye kero ambazo zipo katika uwezo wa kutatuliwa na wateule wake kama wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri, basi atawafukuza kazi.

Hii inathibitisha nia ya dhati ya Rais ya kuhakikisha dhamana aliyopewa ya kuwatumikia wananchi na kutatua kero zao, inafanikiwa bila vikwazo.

Uongozi wa kiutumishi umedhihirika pale Rais Samia alivyoshughulikia changamoto ya watumishi wa umma kutopanda vyeo na madaraka kwa muda mrefu.

Akizungumza na watumishi wa umma wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deo Ndejembi, anabainisha kuwa tangu serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia iingie madarakani zaidi ya watumishi wa umma 180,000 wamepandishwa madaraja.

Hii imeongeza ari ya watumishi kufanya kazi kwa bidii na kujituma zaidi. Vilevile, kiongozi mtumishi huandaa vikao na mikutano ili kukutana na makundi mbalimbali kujua changamoto zao na kupokea maoni yao ili kuyafanyia kazi.

Juni mwaka jana Rais Samia alizungumza na vijana wa Mwanza katika Uwanja wa Nyamagana kwa niaba ya vijana wote nchini ikiwa ni mwendelezo wa kusikiliza kero za makundi ya watu mbalimbali katika jamii.

Aidha, Mei 2021, Rais Samia alikutana na wazee wa Dar es Salaam takriban 900 katika ukumbi wa Mlimani City kwa niaba ya wazee wote akiwahakikishia kuzifanyia kazi changamoto zao kama vile kupata matibabu, kulipwa pensheni, kupata wawakilishi katika Baraza la Madiwani na bungeni.

Halikadhalika, kiongozi mtumishi ana sifa ya kukataa kutukuzwa pale anaposifiwa kupitiliza kutokana na mambo mazuri aliyofanya. Katika sherehe za Jubilei ya miaka 25 ya uaskofu wa Askofu Severine Niwemugizi wa Jimbo la Rulenge-Ngara mkoani Kagera, Askofu Niwemugizi anamshauri Rais Samia kukataa kwa namna yeyote ile kulinganishwa na Mungu.

Akitoa ufafanuzi wa ushauri huo, Rais Samia, anasema kuwa hana tabia ya kutukuzwa wala kulinganishwa na Mungu, anajitahidi kuwa na hekima na uvumilivu wa kusikiliza maoni ya wengine kwani hiyo ndiyo kanuni ya uongozi bora.

"Baba Askofu umeniasa mambo ya kukataa kutukuzwa na mimi nataka nikuahidi mbele ya umma huu kwamba, hiyo si tabia yangu na ninajitahidi kujishusha niwe sawa na wengine, maana utumishi huu kama mpango wa Mungu ulivyo ameniweka hapa niwatumikie na sio kujitukuza kwenu. Nitajitahidi na Mungu anisaidie kuwa na hekima na uvumilivu na niwe na sikio la kusikiliza yale yanayosemwa na wengine, nashukuru sana Baba Askofu kwa maneno haya," alisema Rais Samia.

HABARI KITAIFA

## Watakiwa kupaza sauti kuhusu ukatili

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KUTOKANA na kuripotiwa kwa matukio ya vitendo vya ukatili katika maeneo mbalimbali hapa nchini Kituo cha Msaada wa Kisheria Kibaha (KPC), kimewataka wananchi kutoa ushirikiano kwa taarifa zinazohusu vitendo hivyo ili vikomeshwe.

Hayo yalisemwa jana mjini hapa na Humphrey Munuo kwa niaba ya Mkurugenzi wa KPC wakati wa utoaji wa elimu ya kukabili vitendo vya kikatli kwa wananchi wa kata ya Mkuza wilayani Kibaha.

Munuo alisema moja ya vikwazo ambavyo vinasababisha kuendelea kwa matukio hayo ni jamii kukaa kimya kwa kutoripoti vitendo hivyo.

Alisema ili kupunguza matukio ya ukatili ndani ya jamii, moja ya njia ni kuyasema kwa kutoa taarifa kwenye vyombo vinavyohusika badala ya kukaa kimya na kusababisha ukatili kuendelea kwenye jamii.

Kwa mujibu wa Munuo, vitendo vya ukatili ambavyo ni pamoja na vipigo, ubakaji, ulawiti, kuchoma moto na vile vinavyoambatana na hivyo, husababisha jamii kuona kuwa ni vitu vya kawaida na kufanya hali ya ukatili kukua zaidi.

"Matukio ya ukatili ni mengi, lakini jamii imekuwa ikikaa kimya na kufumbia macho kwani ukatili huanza kidogo kidogo na kama hatua hazijachukuliwa husababisha mauaji," alisema.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari Nyumbu, Fredrick Chagoha, alisema njia nyingine ya kukabili vitendo hivyo ni watu kuwa na hofu ya Mungu na kuweka hisia za mambo mazuri kwenye mioyo yao.

Chagoha ambaye ni mtaalamu wa saikolojia alisema mtu anapowaza mambo mabaya, ndivyo yanavyosababisha kufanya vitendo vibaya vikiwamo ukatili na mauaji ambavyo hutokana na mvuto wa mawazo mabaya.

Naye mkazi wa Mkuza, Martha Mola, alisema wanajamii wamepata uelewa kwa kuwa walikuwa hawajui baadhi ya vitendo kuwa ni ukatili.

Mola alisema baadhi ya wanajamii wamekuwa waoga kutoa taarifa za vitendo hivyo wakiwamo wanawake ambao hujitwika uvumilivu na kusababisha vitendo hivyo kuzidi kukua.

# Wananchi wamwomba Rais kuingilia mgogoro wa ardhi kati yao na JWTZ

**Na Maulid Mmbaga**

WANANCHI wa Mtaa wa Kijaka Kimbiji, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni Dar es Salaam, wametoa malalamiko kwa Rais Samia Suluhu Hassan na kumwomba kuingilia kati mgogoro wa ardhi ambao umedumu zaidi ya miaka 15 kati yao na Jeshi la Ulizi la Wananchi Tanzania (JWTZ).

Akizungumza na gazeti hili, Mwenyekiti wa kamati iliyoteuliwa na wana Kijaka kwa ajili ya kufuatilia suala hilo, Maiko Chanzo, alisema wamekuwa katika mgogoro wa ardhi na jeshi hilo tangu miaka ya 2000 baada ya kutakiwa kuondoka bila fidia katika eneo alilodai kuwa ni mali yao.

Msemaji wa JWTZ, Luteni Kanali Gaudentius Illonda, alipoulizwa na gazeti hili kuhusu jambo hilo alisema hakuwa na taarifa ya suala hilo huku akidai kuwa hakuna mgogoro kati yao na wananchi.

"Kazi ya jeshi ni kumwondoa adui katika ardhi ya mwananchi na sio kumwondoa mwananchi katika ardhi yake na sikuwa na taarifa kuwa kuna mgogoro kama huo, lakini nitafuatilia baada ya hapo nitatoa majibu," alisema Illonda.

Chanzo alibainisha kwamba eneo hilo lina ukubwa wa hekta 1,557 sawa na ekari 3,892 ambalo ramani yake ilisajiliwa kwa Na 45476. Pia alidai kuwa miaka ya 2000 Jeshi hilo liliomba kutumia sehemu hiyo kwa lengo la kutumika kama eneo la mafunzo na mazoezi kwa vikosi vya kamandi ya maji.

Alisema baada ya muda jeshi hilo lilihitaji kumiliki eneo hilo akidai kuwa wananchi wote walioko ndani ya eneo husika walitakiwa kushiriki katika zoezi la kufanyiwa tathmini ya mali zao kwa ajili ya kulipwa fidia ili waondoke.

"Mwaka 2004 tulipewa taarifa na uongozi wa halmashauri kuwa tujiandae kufanyiwa tathmini ya mali zetu zilizoko ndani ya eneo hili ili tulipwe fidia, lakini hadi sasa hatujalipwa na badala yake tunalazimisha tuondoke wakati tulimiliki ardhi katika eneo hilo kihalali kwa kufuata taratibu zote," alidai na kuongeza.

"Familia zetu zipo ndani ya eneo hilo na tumekatazwa tusifanye shughuli yoyote ya kimaendeleo ikiwamo kilimo jambo ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa kuzidisha ugumu wa maisha, sisi hatujakataa kuondoka, lakini tunahitaji tulipwe fidia kwasababu eneo hili ni mali yetu na hati za umiliki tunazo," alidai Chanzo.

Alidai kuwa chanzo cha mgogoro ni baada ya jeshi hilo kuwabadilikia na kudai kuwa eneo hilo ni mali yao huku akihoji kwamba kama lilikuwa ni mali yao kwanini mwanzo walipotaka kulitumia waliomba kibali na kuanzisha mchakato wa kutaka kuwalipa ambao alidai kuwa haukukamilika hadi sasa tangu 2004.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Kigamboni Faustine Ndugulile, alisema "Naufahamu mgogoro huu, ninafuatilia suala hili na Wizara ya Ulinzi, mara ya mwisho kuwasiliana na wizara ilikuwa ni Ijumaa iliyopita," alisema Ndugulile.




Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi (katikati), akikabidhi taarifa ya mradi wa uboreshaji maji kwa Mkoa wa Dar es Salaam kwa Mkurugenzi wa Bonde la Mto Ruvu, Elibariki Mmasy, wakati wa uzinduzi wa mradi huo jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi wa WWF, Dk. Aman Ngusaru na Mkurugenzi wa TBL, Jose Moran. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TBL yatoa bil. 1.3/- kuboresha upatikanaji maji

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya Bia Tanzania (TBL), imetoa Sh. bilioni 1.3 kwa ajili ya mradi wa kuboresha upatikanaji wa maji katika mkoa wa Dar es Salaam.

Mradi huo ulizinduliwa jana Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi na utatekelezwa na Bonde la Wami/Ruvu (WRBWB) kwa ushirikiano na Shirika la Kimataifa la Wanyamapori Duniani (WWF).

Mkurugenzi wa Bonde la Wami/Ruvu, Elibariki Mmassy, alisema mradi huo unalenga kuboresha ubora na wingi wa maji pamoja na kulinda viumbe hai katika maeneo ya vyanzo vya maji Dar es Salaam.

Alisema uanzishaji wa mradi unaendana na kanuni na mbinu ya usimamizi jumuishi wa rasilimali za maji ili kuhakikisha uratibu wa maendeleo ya rasilimali za maji kwa nia ya kuboresha ustawi wa kijamii na kiuchumi bila kuathiri uendelevu wao.

Mmassy alisema mradi unachangia katika kufanikisha juhudi za WWF za majisafi na matokeo ya uhifadhi kama vile mpango wa Blue Heart of Africa (BHoA), ambao unalenga kuhakikisha kwamba rasilimali za majisafi za Afrika zinasimamiwa na kuhifadhiwa ipasavyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TBL, Jose Moran, alisema mradi huo unatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia Machi, mwaka huu hadi Desemba, 2025. Pia alisema utafanyika kimkakati kupitia malengo ambayo yameandaliwa ili kuchangia upatikanaji wa uhakika wa maji salama Dar es Salaam na malengo ya uhifadhi.

Alisema mradi huo utatekelezwa katika vitongoji vidogo vitatu vikiwamo Msimbazi, Mzinga na Ruvu Chini ambavyo vinachukua takribani eneo la kilomita za mraba 18,000 ambazo zinatumika katika usambazaji wa maji na huduma za kimazingira kwa takribani watu milioni 6.5.

"Kutokana na mradi huu, inatarajiwa kuwa jamii iliyo katika eneo la mradi kando ya kitongoji cha Msimbazi, Mzinga na Ruvu Chini itapata maji ya bomba katika vijiji vyenye shida ya maji na kupunguza matukio ya mmomonyoko wa maji katika eneo la vyanzo vya maji," alisema. "Washirika wote wa mradi huu wameungana ili kuhakikisha malengo makuu matatu ya kimkakati ambayo ni kuboresha ubora na wingi wa maji katika mito muhimu ya vyanzo vya maji vya Dar es Salaam ifikapo mwaka 2022," aliongeza.

Pia alisema lengo ni kuboresha usimamizi na urejeshaji wa miradi midogo midogo tegemezi na uboreshaji wa vyanzo vya maji ifikapo mwaka 2024 ili kuboresha kiwango cha suluhisho za asili. Mkurugenzi wa WWF, Dk. Amani Ngusaru, alisema mradi huo utafanikiwa kupitia juhudi za ushirikiano wa wananchi na wadau wa maendeleo.

Naibu Waziri Mahundi alisema mradi wa maji salama utasaidia kwa kiasi kikubwa kushawishi wadau mbalimbali kufanya kazi kwa pamoja ili kuandaa mbinu shirikishi za kukabiliana na hatari za maji.

Alisema hiyo itachangia katika kuboresha ubora na wingi wa maji pamoja na kuboresha maisha ya jamii za wenyeji katika maeneo ya vyanzo vya maji.

# Uharibifu vyanzo vya maji washtua

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, ametaka vyanzo vya maji katika Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini vilindwe kwa nguvu kubwa kwa maelezo kuwa kupungua kwake ni hatari kwa usalama wa nchi.

Pia amewashauri wadau wote wa uhifadhi wa maji katika Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini kutumia mbinu mbalimbali na kufikisha elimu kwa wananchi wa ngazi ya chini wajue umuhimu wa kutunza vyanzo hivyo.

Gaguti alitoa angalizo hilo jana mkoani hapa wakati akifungua kikao cha Jukwaa la Wadau wa Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini, na kusema miaka 20 iliyopita katika maeneo tofauti, kulikuwa na mito na mifereji ya maji ambayo sasa zimetoweka.

Aliongeza kuwa mahitaji ya maji yanaendelea kuongezeka, huku vyanzo vyake vikiwa vinaendelea kutoweka, hali aliyoeleza inaweza kusababisha mgogoro kati ya wananchi na serikali ikiwa maeneo tengefu ya uhifadhi wa maji ardhini hayatalindwa.

"Kwa wananchi mmoja mmoja uelewa wa maji ni mdogo, wao maji ni yale wanayoyaona juu ya mgongo wa ardhi yakitumika, yaliyo ardhini hawana habari nayo... sasa ni jukumu letu kwa pamoja kufikisha elimu ya namna ya uhifadhi mpaka ngazi ya chini kabisa ya mtu mmoja mmoja, tusipokuwa makini tutaingia kwenye mgogoro na watu watakaovamia maeneo tengefu," alisema Gaguti.

Mkurugenzi wa Maji Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini, Sudi Mpemba, alisema dhamira kuu ya jukwaa hilo ni kuwakutanisha wadau wa sekta mtambuka kuzungumza na kukubaliana namna bora yenye ufanisi na uendelezaji wa rasilimali za maji.

Aliongeza kuwa katika kikao hicho kuzungumza na kuja na suluhisho juu ya namna ya kutumia rasilimali za maji kwa matumizi ya sasa na baadaye katika hali ya uendelevu.

"Bonde mpaka sasa tumeshaainisha vyanzo vipatavyo 58, kati ya hivyo vyanzo tisa vimehifadhiwa na kuwekewa mipaka kama chanzo cha Mbwinji kinachotumiwa na Mamlaka ya Maji Masasi na Nachingwea (MANAWASA), lakini kuna chanzo cha Mitema, ni chanzo chenye maji ya kutosha na kinategemewa na wakazi wa mji wa Newala na kinatumiwa na Mamlaka ya Makonde... hiki tumeshafanyia uhifadhi na shughuli za uhifadhi,"alisema Mpemba.

Alisema licha ya jitihada za Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini kuhifadhi na kulinda kila chanzo cha maji, kuna maeneo vyanzo hivyo vimeharibiwa, na kuvitaja baadhi ni maeneo ya Wilaya ya Mbinga ambapo wameshaanza kuchukua hatua na kuzuia shughuli zinazosababisha uharibifu.

Katibu Mkuu mstaafu Wizara ya Maji na Mwenyekiti wa Jukwaa la Wadau wa Rasilimali za Maji Taifa, Mhandisi Mbogo Mfutakamba, alieleza kuwa sekta ya maji imeshika nafasi kubwa ya uchumi wa Taifa, na kutolea mfano matumizi ya dola moja kwenye maji inaweza ongeza hadi dola 4 kwenye uchumi wa nchi.

Awali Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimali za Maji wa Wizara ya Maji, Peter Kishiwa, aliyemwakilisha Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji nchini, Dk. George Lugomela, alisema sera ya kwanza ya Taifa ya maji ya mwaka 1991, iliyoboreshwa na sera ya 2002 inatoa msisitizo wa ushirikishaji jamii katika kupanga na kutekeleza miradi ya maji pamoja na usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji.

Alisema rasilimali za maji zilizoko nchini kwa sasa ujazo wa mita za mraba bilioni 126 na kati ya hizo bilioni 105 zipo juu ya mgongo wa ardhi na chini ya ardhi kuna ujazo wa mita za mraba bilioni 21.



Wakulima wa zao la chai wa Igoda, Kata ya Luhunga wilayani Mufindi, mkoani Iringa, wakipima majani ya chai jana, kwa ajili ya kuuza kwenye viwanda vya uchakataji chai ambapo kilo moja ya majani mabichi inauzwa 12/-. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Wizara za kisekta zahimizwa bajeti utekelezaji programu makuzi watoto

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WIZARA za kisekta zimehimizwa kutenga Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/23 ili kutekeleza Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Watoto (PJT-MMMAM).

Hayo yalisemwa jana jijini hapa na Mkurugenzi wa Sera na Mipango katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Sayi Magesa, katika ufunguzi wa kikao cha Kikosi Kazi cha Taifa cha Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kwa niaba ya Katibu Mkuu, Dk. Zainab Chaula.

Magesa alisema ili kuhakikisha afua za utekelezaji wa programu hiyo zinatekelezwa, lazima wizara zijumuishe afua hizo kwenye mpango wa bajeti.

Alisema programu hiyo imeandaliwa kwa ajili ya kutatua changamoto zilizokuwapo pamoja na kuharakisha upatikanaji wa matokeo chanya katika utoaji wa huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kwa kuhusisha sekta zote zinazohusu afya, lishe, ujifunzaji wa awali, malezi yenye mwitikio, ulinzi na usalama wa mtoto nchini.

"Katika hili la kutenga bajeti, niwatake pia wadau wa maendeleo mwongeze uwekezaji katika kutekeleza afua za Programu Jumuishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ili kuongeza kasi kwenye utekelezaji wa programu hii," alisema.

Magesa pia alisema utekelezaji wa programu hiyo umesaidia uratibu wa afua zilizopo katika upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi katika kuboresha utoaji wa huduma za malezi na makuzi ya watoto.

Mkurugenzi wa Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto Tanzania, Mwajuma Rwebangira, aliwaomba wadau kuendelea kujitokeza kushirikiana na serikali kuhakikisha Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto inatekelezeka na kuleta matokeo chanya katika jamii.

Naye Mwakilishi wa Shirika la Bright Jamii Initiatives, Godwin Mongi, alisema Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto imelenga hasa kuifikia jamii hasa wazazi, walezi na watoto katika kuhakikisha suala la malezi linakuwa ni la umuhimu ili kusaidia kupata watoto watakaoleta mabadiliko na maendeleo katika jamii zao.

Akizungumza katika kikao hicho, Mwakilishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Kija Bank, alisema wizara hiyo kupitia Jeshi la Polisi itahakikisha watoto wanalindwa dhidi ya vitendo vya ukatili tangu wakiwa wadogo na kuwataka wazazi kuchukua hatua za kuwalinda watoto dhidi ya ukatili kwa kutimiza jukumu la malezi.

Hivi karibuni, serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, ilizindua Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto.

# Madiwani wa Namtumbo wamkataa ofisa ununuzi

**Na Gideon Mwakanosya,** NAMTUMBO

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma, limemkataa ofisa ununuzi wa halmashauri hiyo kwa madai ya kuchelewesha ununuzi wa vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

Akitoa uamuzi huo juzi , Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Juma Pandu, alisema madiwani hawamtaki ofisa huyo, hivyo atafute halmashauri nyingine ya kufanyia kazi na si Namtumbo.

Pandu alisema uamuzi huo umefikiwa na baraza hilo baada ya madiwani kukilalamikia kitengo hicho kwa muda mrefu juu ya ucheleweshaji wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi bila kuwapo mabadiliko.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Dk. Julius Ningu, aliwaagiza madiwani katika salamu zake za serikali katika baraza hilo kuwa wanatakiwa kuchukua uamuzi mgumu katika kitengo hicho cha ununuzi kwa kuwa kimekuwa kero kwa wananchi katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

"Nimefanya ziara ya kukagua miradi ya ujenzi wa vyoo katika zahanati wilaya nzima ya Namtumbo kero kubwa inaelekezwa kitengo cha ununuzi kuchelewesha ununuzi wa vifaa, "alisema.

Ofisa Ununuzi huyo, Samson Manjale, alipohojiwa juu ya uamuzi huo akiwa ukumbini hapo, alisema alitegemea kuwapo kwa uamuzi huo kutokana na misimamo yake ya kusimamia miongozo ya serikali kwa kutowapa kazi baadhi ya madiwani waliomba kujenga baadhi ya majengo.

Aliyataja baadhi ya majengo ambayo madiwani waliyaomba kujenga kuwa ni ya kituo cha afya Magazini, hospitali ya wilaya na vyoo vya zahanati na kushuhudia upinzani mkali wa kutaka kumwondoa katika halmashauri hiyo.

Manjale alisema suala la kukilalamikia kitengo cha ununuzi kuchelewesha ununuzi si kweli kwa kuwa yeye haandiki dokezo la kuomba vifaa bali idara na wakuu wa zahanati zinazotekeleza mradi kuwahisha maombi, hivyo kitengo cha ununuzi kushirikiana na idara ya ujenzi kujiridhisha vifaa vinavyotakiwa kununuliwa kisha idara ya fedha kumlipa mzabuni kwa wakati.

"Kwa kawaida mzabuni anatakiwa kutoa huduma ya vifaa kabla ya kulipwa fedha zake. Sasa katika halmashauri yetu wazabuni wanatoa huduma halafu fedha zao hawalipwi kwa wakati, hivyo kitengo cha ununuzi kinapata wakati mgumu kuwaomba wazabuni kuendelea kutoa huduma wakati madai yao mengine ya nyuma hayajalipwa," alisema.

## Balozi ataja mbinu kunufaika mpakani

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

BALOZI wa Tanzania Malawi amewataka wananchi wanaoishi mpakani wilayani Ileje mkoani Songwe na Wilaya ya Chitipa, Malawi, kuimarisha uhusiano ili kufungua fursa za kiuchumi kwa mataifa hayo mawili.

Benedicto Mashimba alitoa rai hiyo jana baada ya kutembelea mpaka wa Tanzania katika mji mdogo wa Isongole wilayani Ileje na kupokea taarifa ya hali ya mpaka kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Anna Gidarya.

Mashimba alisema katika kuhakikisha mpaka huo unafungua fursa za kiuchumi na kibiashara, serikali ya Malawi ina mpango wa kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita zaidi ya 30 kutoka Chitipa mpaka Daraja la Mto Songwe ikiwa ni sehemu ya mpaka wa nchi hizo mbili.

Alisema ili kuondoa adha ya usafiri kwa upande wa Chitipa, Serikali ya Tanzania imejenga barabara yenye urefu wa zaidi ya kilomita 50 kutoka mpakani huko hadi Mpemba na kurahisisha kusafirisha mizigo.

"Wafanyabiashara wa Malawi hupata shida kusafirisha mizigo yao kutoka Tanzania pindi wanapotoka kununua mizigo Tanzania katika boda ya Tunduma na Isongole, hivyo nitaishauri Serikali ya Malawi kuhakikisha wanatatua changamoto hiyo," alisema Mashimba.

Alipongeza uhusiano mzuri ulioko baina ya wilaya hizo jirani katika huduma za kijamii kama vile afya ambapo wananchi hupata huduma za afya kwa kutumia Hospitali ya Itumba iliyoko wilayani Ileje na Hospitali ya Chitipa iliyoko wilayani Chitipa, Malawi.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, alimhakikishia balozi huyo kuwa serikali itahakikisha wanashirikiana na wananchi kuimarisha usalama mpakani hapo, ikiwa ni pamoja na kuendeleza na kutafuta fursa zitakazokuza uchumi wa wananchi wa Ileje na taifa kwa ujumla.

Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Anna, alisema uhusiano mzuri baina ya mataifa hayo mawili hususani mpaka wa Isongole na Chitipa umetokana na vikao vya ujirani mwema na wilaya za Chitipa - Malawi vilivyotatua kero kadhaa za pande mbili.

"Katika kukuza uchumi kwa wananchi serikali ipo katika mpango wa kujenga kituo cha ushuru wa forodha katika Mji wa Isongole, ili kukuza fursa za biashara za mpakani sambamba na kuongeza mzunguko wa fedha kama ilivyo boda zingine Tanzania kama vile Boda ya Tunduma wilayani Momba mkoani Songwe na boda ya Kasumulu wilayani Kyela mkoani Mbeya," alisema Anna.

# 'Bima za afya sasa zitoe huduma magonjwa yote yasiyoambukiza'

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imeombwa kuziingiza huduma zote za magonjwa yasiyoambukiza katika bima ya afya ili kuwaondolea matatizo wagonjwa.

Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA), Prof. Kaushik Ramaiya, aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa uzinduzi wa mkakati wa utetezi kuhusu bima ya afya kwa wote inayojumuisha magonjwa yasiyoambukiza.

Mkakati huo uliandaliwa na TANCDA na kushirikisha wadau wakiwamo Wizara ya Afya, wajumbe wa kamati ya kudumu ya Bunge ya masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Dawa za Kulevya na Magonjwa yasiyoambukiza, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza na wahariri wa vyombo vya habari.

Akizungumza katika uzinduzi huo Ramaiya alisema, "Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya una bima za aina mbalimbali ambazo zimekuwa zikitoa huduma za matibabu ya magonjwa yasiyoambukiza pamoja na magonjwa mengine, lakini baadhi ya huduma za matibabu hazipatikani katika bima hizo."

Alisema magonjwa yasiyoambukiza yana gharama kubwa katika kuyatibu na wananchi wamekuwa wakikata bima za afya, lakini kadi hizo zimekuwa zikitoa baadhi ya huduma.

"Ninaiomba serikali iliangalie hili kwani tathmini iliyofanywa na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) inaonyesha baada ya miaka mitano hadi 10 ijayo vifo vinavyotokana na magonjwa yasiyoambukiza vinaweza kuongezeka na kuwa zaidi ya asilimia 55," alisema.

Alisema magonjwa yasiyoambukiza yasipotibiwa vizuri husababisha mtu kupata madhara mengine kama vile figo, mishipa ya damu, macho, kiharusi na madhara mengine mengi ambayo husababisha kifo.

"Serikali iratibu upatikanaji wa matibabu ya magonjwa haya katika maeneo yote yenye zahanati na vituo vya afya ili jamii iweze kupata huduma ya karibu na kwa wakati hii itapunguza madhara yanayoweza kutokea kama magonjwa haya hayatatibiwa mapema," alisema.

Mbunge wa Mbozi Mkoa wa Songwe, George Mwenisongole, alisema suala la bima ya afya kwa wote likawe ajenda ya kitaifa ili kutoa fursa kwa kila Mtanzania kuwa na matumaini ya kupata matibabu pale wanapougua magonjwa mbalimbali.

"Bima ya afya kwa wote inapaswa kuwa bima isiyobagua lakini bima inayotoa huduma zote za matibabu ili Watanzania wafaidike na huduma za matibabu hasa wenye magonjwa yasiyoambukiza ambayo yamekuwa yakitibiwa kwa gharama kubwa."



Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui (kushoto), akimvisha medali ya heshima Mwenyekiti wa Makampuni ya Simba Group, Jitesh Jayantilal Ladwa, kwa niaba ya Rais wa nchi hiyo kutokana na ushirikiano mzuri wa kibiashara kati ya kampuni hiyo na Ufaransa, katika hafla iliyofanyika nyumbani kwa balozi huyo, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tanzania yawasilisha ujumbe mazingira UN

**Mwandishi Wetu,** NAIROBI

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, ameshiriki katika ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEA 5) unaofanyika jijini Nairobi, Kenya.

Katika ufunguzi wa mkutano huo juzi, Khamis aliwasilisha ujumbe maalumu wa Tanzania kuhusu mazingira, akibainisha jitahada za Tanzania zilizochukua katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Alizitaja jitihada hizo kuwa ni pamoja na kupambana na uharibifu wa mazingira unaotokana na mifuko ya plastiki, akisema kuwa ili kukabiliana na tatizo hilo, Tanzania imechukua hatua za kupiga marufuku uzalishaji, uingizaji na matumizi ya mifuko hiyo. Naibu Waziri huyo alisema kuwa mwaka 2019 Tanzania ilitunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa katazo la mifuko ya plastiki huku akieleza kuwa ili kufanikiwa, unahitajika ushirikiano madhubuti wa kimataifa ikiwamo kuwa na sera ya pamoja na hatua madhubuti za pamoja za kuhakikisha dunia inakuwa salama.

Alisema katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Tanzania imeendelea kutekeleza wajibu wake kama ilivyojieleza katika Mchango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (NDC) pamoja na Mkakati wa Kupambana na Mabadiliko ya Tabianchi (NCCRS) wa mwaka 2021-2026.

Naibu Waziri Khamis alisema kuwa mbali ya jitihada hizo, Tanzania pia imeendelea kuimarisha uwezo wa nchi kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Takriban mataifa 193 wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) yamepitisha maazimio yanayolenga kubuni makubaliano mwafaka ya kutokomeza taka za plastiki kwa kupunguza matumizi yake kutoka vyanzo vyake hadi baharini.

Wajumbe wa mkutano huo wanatarajia kufikia uamuzi wa pamoja katika hatua za mwanzo za kukabiliana na uchafuzi wa mazingira unaotokana na mifuko ya plastiki ambayo inatajwa kama chanzo kikubwa cha uchafuzi wa mazingira.

Kwa mujibu wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), zaidi ya chupa za plastiki milioni moja hununuliwa kila dakika kote ulimwenguni kwa matumizi ya maji ya kunywa huku mifuko ya plastiki zaidi ya trilioni tano ikitumiwa kila mwaka duniani.

Mkutano wa UNEA 5 uliofunguliwa Februari 28, unatarajiwa kuhitimishwa leo, ukijumuisha wajumbe mbalimbali wakiwamo mawaziri na wadau mbalimbali wa mazingira duniani.

# Madiwani wote Musoma wapata chanjo UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

MADIWANI wote 28 wakiwamo saba wa viti maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma mkoani Mara, wamepata chanjo ya kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19. lakini kama njia ya kuhamasisha jamii kupata huduma hiyo.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Charles Magoma, alisema hayo, alipokuwa akizungumza na gazeti kuhusu mikakati ambayo imewekwa na halmashauri yake kwa ajili ya kufanikiwa chanjo ya ugonjwa huo.

"Sisi madiwani wote wa kata 21 na saba wa viti maalum tumeshapata chanjo ya ugonjwa huo na sasa tunaendelea na kampeni ya kuhamasisha chanjo ndani ya jamii, kila diwani katika eneo lake," alisema Magoma.

Akielezea jinsi ambavyo madiwani wote wamechanjwa, mwenyekiti huyo alisema, kila kikao cha baraza la madiwani, watu wa huduma hiyo huwa wanakuwapo kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu chanjo.

"Katika mazingira hayo, madiwani wote wamechanjwa, na bado watoa huduma wanaendelea kuwapo katika vikao ili kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha ili kila anayehudhuria vikao vya baraza achanje," alisema.

Mbali na madiwani hao kuchanja, Magoma alisema kampeni za chanjo zinaendelea katika maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye minada, masoko, myalo na nyumba kwa nyumba.

"Tumejiwekea utaratibu, kila diwani anapofanya ziara ya kukagua shughuli za maendeleo katika kata yake, anaambatana na watu wa chanjo wanashirikiana kuhamasisha chanjo, mtu anayekuwa tayari anachanjwa," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema, kwa utaratibu huo, watu wanaendelea kufikiwa katika vitongoji vyote 374, vijiji 68 na kata 21 zinazounda halmashauri hiyo ya wilaya za Musoma, na kwamba wamehamasika.

Alisema, Baraza la Madiwani la halmashauri hiyo, linazingatia maelekezo ya Wizara ya Afya ambayo yanalenga kuifanya kampeni ya chanjo ya UVIKO-19 kuwa shirikishi ili kuhakikisha ugonjwa huo unatokomezwa nchini.

"Madiwani kuzunguka na watoa huduma ya chanjo katika ziara za kukagua shughuli za maendeleo, ni kwa sababu wao (madiwani) si wataalamu wa afya, hivyo ili wananchi wapate elimu sahihi, ni muhimu kuwashirikisha," alisema.

Alisema, madiwani kama wanasiasa, nao wana nafasi ya kushiriki kampeni ya chanjo, kwa kuwa wana ushawishi kwenye jamii wanayoiongoza na kwamba kwa njia hiyo anaamini mchango wao ni mkubwa.

"Kama umewahi kusikia, taarifa za Wizara ya Afya, Mkoa wa Mara ni moja ya mikoa mitano inayofanya vizuri kwenye chanjo ya corona, ninaamini madiwani wa halmashauri yetu watakuwa wamechangia katika hilo," alisema.



Washindi wa promosheni ya Vodacom Shangwe Lipo Pale Pale, Miraji Zubery (wapili kushoto) na Faustine Boay (wapili kulia) wakazi wa Babati, wakiwa na zawadi zao za smart Tv, baada ya kukabidhiwa na Meneja Mauzo Mwandamizi wa Vodacom Kanda ya Kaskazini, Nathan George (kulia), akishirikiana na Meneja Mauzo, Nanyaro Kaanankira (watatu kushoto), mjini Babati, mkoani Manyara juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC awatuliza wananchi maziko waliopigwa radi

**Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, jana aliongoza maziko ya watu saba waliokufa kwa kupigwa na radi wakiwa katika shughuli za kilimo.

Akiwa katika kijiji cha Milundikwa Kata ya Nkandasi, Mkirikiti aliwataka waombolezaji na wafiwa kuliona tukio hilo kama ni ajali ya kawaida na wamwombe Mungu awape subira katika kipindi hicho kigumu.

Alisema kuwa msimu wa mvua za masika huwa zinaambatana na radi, hivyo ni vizuri wananchi wakaendelea kuchukua tahadhari, kwani radi ni ajali na inaweza kupiga sehemu yoyote. "Ndugu zangu wafiwa na sisi waombolezaji, nawaomba sana muwe na imani kwa mwenyezi Mungu, hii ni ajali kama ajali nyingine, tusianze kutazamana vibaya na kuruhusu mawazo tofauti, tumwombe sana Mungu atufariji na kubwa zaidi tujiandae kila wakati.... tutengeneze maisha yetu, hatujui saa wala siku," alisema.

Alisema ni vizuri kufuata maelekezo ya wataalamu katika kujikinga na majanga mbalimbali ili waendelee kuwa salama kwani maelekezo ya kufuata yapo, hivyo wasiyapuuze.

Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Given Kisantola, alisema kuwa wananchi wa kata hiyo wanahitaji elimu ya vitu gani wafanye wanapoona kuna dalili za mvua zikiambatana na radi.

Alisema wengi wanaamini kuwa radi inapopiga inakuwa imemlenga mtu na imetumwa kwa dhumuni fulani, na kwamba ndiyo maana baadhi yao hawachukui tahadhari wakiamini kuwa haitawadhuru kwa kuwa imelengwa mahusus kwa mtu aliyefanya kosa.

# Bil. 65/- kukarabati Bandari ya Kigoma

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Bandari (TPA) inatarajia kutumia Sh. bilioni 65 kufanya ukarabati wa Bandari ya Kigoma.

Ukarabati huo utajumuisha ujenzi wa sehemu ya kuhifadhi mizigo, kuboresha gati la abiria na kujenga jengo la kisasa kwa ajili ya mapumziko ya abiria.

Meneja wa Bandari ya Kigoma, Manga Gassaya, alibainisha hayo alipozungumza na Sekretarieti ya Korido ya Kati (Central Corridor) walipotembelea bandari hiyo hivi karibuni ili kuona kazi zinazofanyika.

Alisema lengo la kufanya maboresho hayo ni kutoa huduma bora kwa wateja wao wanaopitisha mizigo kwenda nchi za jirani ikiwamo Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC) na kuongeza uwezo wa bandari.

Gassaya alisema fedha kwa ajili ya ukarabati wa bandari hiyo ni ufadhili kutoka nchi ya Japan ambayo imekuwa na uhusiano mzuri na Tanzania.

Alisema maboresho hayo yatachukua mwaka mmoja na nusu hadi miwili, hivyo aliwataka wateja wanaotumia bandari hiyo kujitokeza kupata huduma za uhakika.

Meneja huyo alisema kwa sasa bandari hiyo ina uwezo wa kutoa huduma kwa mizigo tani 300,000 kwa mwaka, lakini baada ya maboresha itakuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa mizigo tani 900,000 kwa mwaka.

Katibu Mtendaji wa Korido ya Kati, Dieudonne Dukundane, aliipongeza serikali kwa maboresho yanayofanyika ili biashara zifike kwenye masoko kwa gharama ndogo.

Alisema lengo lao ni kukuza biashara kwa kuhakikisha wanaunganisha miundombinu ili kuwarahisishia wakulima kufikisha mazao yao sokoni.

**Alisema maboresho hayo yatachukua mwaka mmoja na nusu hadi miwili, hivyo aliwataka wateja wanaotumia bandari hiyo kujitokeza kupata huduma za uhakika.**


Ukurasa 12

**Diplomasia kimataifa inavyopenya mioyo India**




Ukurasa 13

**RUSSIA VS UKRAINE**

**Dunia shakani, 'samaki mmoja' anavyoumiza tenga la wote**



KIPORO CHA MVUTANO CUF

# Waliotimuliwa wahoji kulikoni Ukimya huo Msajili wa Vyama?

• Awajibu wavute subira, majibu yaja

**Na Sabato Kasika**

"NI miezi mitatu tangu tufikishe malalamiko yetu Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Dodoma, lakini hadi leo ni kimya kikubwa kinachosababisha tusijue hatima yetu."

Ni wasiwasi unaotolewa na Abdul Kambaya, mmoja wa viongozi na wanachama waliotimuliwa CUF na kufikisha malalamiko yao kwa Msajili.

Anasema wanatamani kusikia uamuzi wa rufaa yao ili wafahamu hatima yao badala ya ofisi hiyo kukaa kimya tangu kuwasilishwa andiko lao Novemba mwaka jana.

Kambaya aliyekuwa Mkurugenzi wa Habari na Uenezi CUF, na mwana CUF wa karibu wa Mwenyekiti, Profesa Ibrahimu Lipumba, pamoja na wenzake kadhaa walifukuzwa kwenye chama hicho.

"Novemba mwaka jana tuliwasilisha barua ya rufaa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Dodoma, tukilalamika kufukuzwa isivyo kihalali, lakini hadi sasa uamuzi haujatolewa," anasema Kambaya.

Anasema wanachotaka kwa Msajili wa Vyama ni kuomba tafsiri ya ibara zilizokiukwa ndani ya kikao cha Baraza Kuu, lililowavua vyeo na uanachama wa CUF.

"Tangu tupeleke malalamiko yetu kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, Novemba mwaka jana, hakuna uamuzi uliotolewa, tunajiuliza kulikoni?"

**WAAMBIWA SUBIRINI**

Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa Sisty Nyahoza, anakiri kuwa tangu ofisi yao ipokee barua ya malalamiko kutoka kwa wanachama hao, haijatoa uamuzi na kuwataka wavute subira.

"Unapoletewa kesi ni muhimu kuchukua kila hatua za kuhakikisha uamuzi unaoutoa unakuwa wa haki kwa pande zote na siyo kukurupuka , ndiyo maana na sisi hatujatoa uamuzi," anasema Nyahoza.

Anaongeza kuwa haraka haraka haina baraka, na kwamba ofisi inapitia kila hatua zinazotakiwa ikiwa ni pamoja na kusoma vifungu vya katiba ya chama hicho, ambavyo wanachama hao wanadai vimetumika kuwafukuza.

"Ofisi yetu ni mlezi wa vyama, kwa maana ya chama na wanachama wake, hivyo wito wangu kwa hao walioleta malalamiko waendelee kusubiri ufuatiliaji utakapokamilika, watapewa mrejesho," anasema.

Anafafanua kuwa siyo kwamba ofisi yake imekaa kimya, bali inaendelea na mchakato hatua kwa hatua, huku ikijulisha pande zote mbili kinachoendelea ili kuondoa mashaka kuwa huenda kuna upande unaobebwa.

"Niwakumbushe tu kwamba, ofisi yetu inafanya kazi kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zake na siyo matakwa ya kikundi au watu fulani, hivyo wawe wavumilivu, tukikamilisha watajulishwa," anasema .


Msajili wa Vyama vya Siasa , Jaji Francis Mutungi. **PICHA: MTANDAO**

**NI KUTAPATAPA**

Akizungumzia malalamiko ya makada hao kuwa kesi yao inacheleweshwa, Naibu Katibu Mkuu wa CUF, Magdalena Sakaya, anasema, hatua hiyo inaonyesha ni jinsi gani hawana tofauti na mfamaji anayetapatapa.

"Walifikisha malalamiko yao kwa msajili ili kupata haki, lakini wakati haki ikiendelea kutafutwa, wanaanza kulalamika, hii inaonyesha ni jinsi gani wanatapatapa," anadai Sakaya, akisema CUF inaendelea kusimamia haki, kwa kudai kwamba katika uamuzi wa kuwaondoa, hakuna taratibu zilizokiukwa na kwamba chama kitaendelea kuzisimamia bila kuyumba.

"CUF inaamini kuwa Ofisi ya Msajili itatumia katiba ya chama hicho kutoa uamuzi ili kila upande upate haki kwa mujibu wa katiba na si vinginevyo, kwa kuwa ndiyo yenye miongozo yote," anasema.

Anasema pamoja na hao waliofukuzwa, wote kwa pamoja wanasubiri uamuzi wa Ofisi ya Msajili, kwa kufuata utaratibu na siyo kulazimisha.

"Wao ni walalamikaji, sisi ni watuhumiwa, wote tunasubiri maamuzi ya Ofisi ya Msajili, lakini tunashangaa kusikia mara wamekwenda mahakamani kwa jambo ambalo wamepeleka kwa Msajili, wanatapatapa, " anaongeza Sakaya.

**MGOGORO ULIVYO**

Mwaka jana, makada 10 wa CUF, waliitisha kikao na waandishi wa habari wakielezea kutoridhishwa na hatua zinazochukuliwa na Baraza Kuu la chama hicho la kuwavua vyeo na uanachama.

Baada ya kuzungumza na vyombo vya habari, kuelekea mwishoni mwa Novemba mwaka jana, walilalamika walitinga Ofisi ya Msajili wakitaka tafsiri ya uamuzi wa kikao kilichowatimua.

Walidai kuwa kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu na kwamba uliotumika haukufuata misingi ya katiba ya chama ikiwamo kutotimia kwa akidi ya wajumbe na kuwapo wajumbe feki katika kikao cha chama hicho.

Baadhi ya makada hao ni Makamu Mwenyekiti wa CUF Zanzibar, Mussa Haji Kombo, aliyekuwa mgombea mwenza wa urais 2020, Hamida Abdallah Weshi na Mjumbe wa Baraza Kuu Abdul Kambaya.

Ofisi ya Msajili ilithibitisha kupokea malalamiko yao, na kuiambia Nipashe kuwa iliiandikia CUF barua kujibu malalamiko ya wanachama wake waliofukuzwa.

# Neema diplomasia ya uchumi inavyopenya mioyo India

• Wawekezaji waja kwenye gesi, matibabu kibingwa



Rais Samia Suluhu Hassan, katika ziara ya nchi za ughaibuni hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa India nchini, Binaya Pradhan, anasema Tanzania inabadilika inavaa sura mpya kidiplomasia ya kimataifa na ya kiuwekezaji hatua inayoivutia nchi yake.

Anaona imefanya mabadiliko anayoyaita chanya ambayo yanatoa mweleko mpya kwenye uwekezaji unaodumisha na kuimarisha uhusiano wa kidipolomasia baina ya nchi hizo, lakini pia kugusa uwekezaji wa vitega uchumi na ushirikiano zaidi.

"India iko tayari na itaendelea kuwa mdau wa Tanzania kiuchumi na kidiplomasia , tunalenga kuanzia sasa kuwekeza kwenye sekta za bandari, kilimo, mafuta, gesi asilia,viwanda vidogo, hospitali pamoja na elimu.

Balozi Pradhan anawaeleza wanahabari jijini Dar es Salaam hivi karibuni, kwenye mkutano wa kuzungumzia masuala ya kiuchumi na kidiplomasia baina ya nchi hizo.

Anasema tangu kuingia uongozini kwa awamu ya sita, mambo mengi yamebadilika kwenye diplomasia ya kiuchumi, akitaja eneo India inalolitazama ni pamoja na uchumi wa bluu.

"Tuna ushirikiano baina ya mataifa yetu na kwenye masuala mengi kubwa ni usalama na ulinzi wa Bahari ya Hindi. "

Anawaambia wanahabari hivi karibuni wataalamu wa bahari 'hydrographers' kutoka India walifika nchini na kufanya savei na utafiti baharini wenye lengo la kufahamu taarifa mbalimbali za bahari kama sakafu yake hali ya maji na uwekezaji.

"Tunatarajia kwa pamoja kuweka ukanda maalumu wa kiuchumi baharini (specific economic zone) baina ya mataifa yetu na mijadala inaendelea."

> Uwekezaji na biashara vinatoa fursa pia kwa mafuta ya karanga, alizeti na matunda kama maembe kutoka Tanzania kuuzwa nchini mwake na kwamba kuna soko kubwa na la uhakika.



Balozi wa India, Binaya Pradhan.

Anasema uwekezaji pamoja na ulinzi utagusa maeneo kadhaa mengine kama kutunza bahari na vitega uchumi kwenye utalii, uvuvi na viwanda vya kuchakata na kufungasha samaki.

Masuala ya kudumisha ulinzi baina ya mataifa hayo yamepewa kipaumbele, na imeundwa kamati ya ulinzi inayoratibu suala hilo na maofisa wa kijeshi wa Tanzania na India, wameshatembeleana anasema Balozi.

Anazungumzia vitega uchumi vya eneo la bandarini kuwa, kampuni kubwa za India za usafirishaji na kuhudumia shehena ziko tayari kuwekeza kwenye bandari za Tanzania.

Anaeleza kuwa India ni mnunuzi namba moja wa bidhaa za Tanzania na kwamba mwaka jana vitu vyenye thamani ya zaidi ya dola bilioni moja vilipelekwa nchini humo.

Anasema hilo lilifanikishwa na kuondoa ushuru kwa bidhaa za Tanzania na kuwataka wafanyabiashara kuuza na kuongeza biashara zaidi kwa sababu ni kama hawana mshindani kwenye soko la India, kwa vile bidhaa hazitozwi kodi.

Balozi Pradhan, anasema wakati matunda kama maparachichi kutoka mataifa mengine yanatozwa kodi ya asilimia 30, ya Tanzania yanaingizwa bure na kuwataka wafanyabiashara kutumia fursa hiyo ya upendeleo maalumu wa 'duty free.'

Anakumbusha kuwa soko la India linapokea mazao mengi kutoka Tanzania akitaja korosho, mbaazi, kunde, dengu, madini na maparachichi yanayoingizwa nchini humo bila ushuru.

Anasema uwekezaji na biashara vinatoa fursa pia kwa mafuta ya karanga, alizeti na matunda kama maembe kutoka Tanzania kuuzwa nchini mwake na kwamba kuna soko kubwa na la uhakika.

Lakini, suala la vikwazo kwa bidhaa za Afrika zinazopelekwa nje, licha ya kupewa heshima ya 'duty free' wafanyabiashara wanalalamikia kuwekewa vikwazo vya kiufundi (technical tariffs) ili kuwakwamisha.

Kwa mfano nchi inaweza kuruhusiwa kupeleka pombe (bia) nje, lakini taifa mnunuzi linaanza kuweka vikwazo vya ufundi kama kutaka ujazo wa robo lita badala ya nusu, maembe au maparachichi yanatakiwa kuwa na ukubwa wanaoupendekeza kwenye kipimo cha kasha au trei zao, yote hayo licha ya bidhaa kuondolewa ushuru, wafanyabiashara wanakwamwa.

Balozi Pradhan, anapoulizwa swali hilo ,anasema, inawezekana kuwepo matatizo ya kiufundi lakini yanatatulika.

Akizungumzia uwekezaji kwenye elimu anasema wafanyabiashara wa nchi yake wana nia ya kuwekeza kwenye ujenzi wa taasisi za elimu nchini na kwamba ina mpango wa kuongeza vituo vya umahiri wa kmpyuta (super computer centres) Chuo Kikuu cha Nelson Mandela na Taasisi ya Ufundi Arusha.

Anasema :"Tunaamini kupitia vituo hivi vya kompyuta Tanzania ina nafasi ya kuendeleza na kufikisha masuala ya elimu mbali zaidi."

Anasema kuwa kituo cha Super computer kilichoko Taasisi ya Ufundi Dar es Salaama –DIT ni mahiri zaidi Afrika na kwamba kuna mambo mengi yanayohusu Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT-TEHEMA) yanayofanikishwa na taasisi hiyo.

Anasema kwenye afya nia ni kuanzisha hospitali zinazotoa huduma za kibingwa ambazo wengi wanazifuata nchini India kila mwaka , wakiamini kuwa ni bora na gharama wanayoimudu.

Balozi Pradhan, anasema India inatamani kufikia Watanzania wengi zaidi na kwamba Ubalozi wake unaandaa ziara mbalimbali za kibalozi mikoani mfano Mwanza, Dodoma na visiwani Zanzibar .

"Kwenye sekta ya afya tunawafikia kwa kusaidia matatibabu mfano kufanikisha tiba za saratani kwenye hospitali za Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Bugando na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza. Lakini pia kufunza wataalamu wa tiba zikiwamo za kibingwa wanaokwenda kujifunza India."

Pradhan, akizungumzia masuala ya huduma muhimu za jamii kama maji, anasema India inashirikiana na serikali kuwekeza kwenye sekta ya maji kwa kuyafikisha kwenye miji mingine mfano inashiriki kwenye ujenzi wa maji kutoka Ziwa Victoria na itaendeleza zaidi ushirika na serikali kwenye miradi ya maji.

Anasema Tanzania na India zimeunda kamati ya pamoja ya maji, ambayo nchi yake itaisaidia kuboresha upatikanaji na usambazaji wa maji nchini.

Anaongeza kuwa licha ya kushirikiana na Tanzania kwenye miradi ya kujenga maji na kuyaongeza mfano Dar es Salaam, wataalamu wa India watashirikiana kuwapa mafunzo wataalam wa maji nchini kwenye utunzaji (water management) mbinu bora za kusambaza maji safi kwa kila mwananchi na uboreshaji wa huduma hiyo muhimu na miundombinu yake.

RUSSIA VS UKRAINE

# Dunia shakani, 'samaki mmoja' anavyoumiza tenga la wote

• Mtikisiko mkubwa kiuchumi, hofu vita vya tatu duniani

Na Gaudensia Mngumi



Wanajeshi wa Russia wakiwa tayari mpakani. **PICHA: MTANDAO**

KILA mahali kuanzia Afrika hadi Amerika, Ulaya na Uarabuni kubwa linalozungumzwa leo ni vita vya Russia na Ukraine (Yukreini). Huenda hoja kubwa ni kwanini Russia ilipige taifa huru na lenye mamlaka na madaraka kamili? Na jingine, hii inaweza kuwa vita vya tatu vya dunia tena vya nyukilia?

Ni dhahiri kila mmoja ana jibu lake na maelezo ya sababu ya uvamizi wa Russia dhidi ya jirani yake. Lakini kwa ujumla ukiangalia wadadisi na wachambuzi wengi wanalitaja suala la Russia kutetea maslahi yake hasa nguvu za jeshi na kutotaka kuingiliwa na NATO ni sababu muhimu.

NATO ambao ni Umoja wa Kujihami wa Ulaya Magharibi na Marekani, wenye wanachama 30 ikiwamo Canada, Ufaransa, Ubeligiji na Marekani ikiwa ndiye baba lao na mwenye teknolojia, jeshi kubwa, fedha na maamuzi muhimu, Russia isingependa kuona ikiingilia.

Ukraine inataka kujiunga na NATO hatua hiyo, inatishia hatima ya Russia na msuli wake kijeshi na nguvu zake. Ni kutokana na sababu kuwa NATO ingeipumulia begani. Inaona kama kumkaribisha adui yako chumbani, hivyo kwa Vladimir Putin, Rais wa Russia, kuruhusu kuwepo na Kamandi ya Jeshi la Marekani kwa jina la NATO, Kyiv mji mkuu wa Ukraine, ulio kilometa 861 kutoka Moscow ni kutishia hatima yake kijeshi na kiusalama.

Umbali huo ni kama kutoka Dar es Salaam hadi Moshi, hatua inayoiweka Russia matatani kwa sababu NATO ambayo Marekani ni baba lao, Putin anaona ikiruhusiwa kuingia Kyiv ni kula na adui yake mwenye lengo la kumtishia na kumdhoofisha.

Wachambuzi wanaona kuwa ndiyo maana anaamua kuipiga, ili aendelee kulinda maslahi yake kijeshi na kama mhimili (polar au super power kwa upande wa Ulaya Mashariki, hasa nchi zilizokuwa kwenye Muungano wa Kisovieti, na asiwe mashakani.

Lakini, kama ilivyo Belarus Ukraine naye ni mtoto kipenzi wa Russia, baada ya kusambaratika, Putin ana maslahi . Na inavyoelekea Rais wa Ukraine Volodymyr Oleksandrovych Zelenskyy, ni jeuri anataka kujiunga na Umoja wa Ulaya na NATO na hataki kumsikiliza Russia kama ambavyo Rais wa Belarus Alexander Lukashenko, anavyofanya.

Mwanzoni Ukraine, ilikuwa eneo muhimu la Russia ikiwa kwenye Umoja wa Soviet, ikizalisha chakula kwa ajili ya mataifa mengi ya Ulaya na kuipandisha chati Russia kiuchumi.

Ilikuwa ni njia ya kusafirisha mafuta na gesi kwenda Ulaya na moja ya nchi inayotumia kwa kiasi kikubwa gesi ya Russia inayopitia Ukraine ni Ujerumani.

Hadi ilipojitenga na Russia kuanzia mwaka 1991, Russia imekua ikiifuatilia kila wakati lakini Rais wake Zelenskyy, hataki na muda wote anaonyesha ari ya kujiunga na washirika wa nchi za Magharibi kama Ulaya, NATO na kuona Russia kama mbabe na mtu asiyemfaa.

Lakini, kwa upande mwingine Ukraine kama nchi yenye uhuru kamili ina haki ya kuamua upande wa kuegemea kujiunga na Umoja wa Ulaya (EU) na NATO, japo ina haki ya kuangalia upande wenye maslahi kitaifa kwa mfano inapata nini kuwa mshirika wa Russia? Kuna faida gani kuwa karibu na NATO na kuiweka Russia njia panda?

Inaweza kuamua isifungamane na upande wowote iwe huru bila kushikana na NATO au EU au Russia iwe na msimamo wa kutaka kuwe na amani badala ya mafarakano kama ilivyo sasa.

Yote hayo ni haki yake na hakuna wa kuilazimisha , hivyo mgogoro huo unabakia zaidi mikononi mwa Ukraine hasa Rais wake Volodymyr Oleksandrovych Zelenskyy.

### KULINDA 'UMWINYI'

Russia inatuhumiwa kuipiga Ukraine ili kukataa demokrasia za Magharibi zisiingie kwenye maeneo yake ya Kisovieti na kuvuruga mifumo yake inayodaiwa ni ya kikandamizaji, kama inavyotazamwa na nchi za kibeberu za Magharibi.

China na Russia ni miongoni mwa mataifa yanayodaiwa na nchi za Magharibi kukandamiza demokrasia kwa kupinga kuwapo uchaguzi huru, haki na wa vyama vingi.

Pia, zinatuhumiwa kupinga haki za binadamu, kubinya uhuru wa vyombo vya habari, kukandamiza asasi za kiraia na kuzia kuwapo kwa uhuru wa maoni tofauti na nchi nyingine kama Marekani na Ulaya.

Russia imeichukua Crimea, inaitawala Belarus kwa ujanja na ingependa kuendelea kuikalia Ukraine ikiamini kuwa kuleta demokrasia za kimagharibi kutabadilisha maisha na kuongeza mitizamo mipya ya kuipinga kutoka kwa wasiotaka umwinyi na ubabe viongozi walioizoea.

Ripoti za mtandao wa gazeti la Global Times, zinaeleza kuwa kwa uzoefu wa China, inaona kuwa demokrasia haiagizwi, kutoka nje siyo bidhaa na siyo suala la kuwafundisha na kuwalazimisha wengine kulikariri.

Inasema badala yake ni lazima ianzie kwenye jamii yenyewe na kuchipuka ndani ya mioyo ya watu wanaohusika ili wawe na amani na furaha kwa kile wanachokubaliana wenyewe, si kulazimishwa.

China imekuwa ikipinga 'modeli' au mifumo ya demokrasia ya Magharibi hasa Ulaya na Marekani ikisema, kwa kuangalia kilichofanyika Afghanistan, Libya na Iraq leo huwezi kulazimisha kupandikiza demokrasia na Marekani ipende isipende imeshindwa.

> Mwanzoni Ukraine, ilikuwa eneo muhimu la Russia ikiwa kwenye Umoja wa Soviet, ikizalisha chakula kwa ajili ya mataifa mengi ya Ulaya na kuipandisha chati Urusi kiuchumi.

Kwa mifano hiyo wanachoona ni maafa kwa wananchi na raia wema wasio na hatia wa mataifa hayo, ambao kila siku wanakufa au kupoteza wapendwa wao kwenye vita na uasi.

China kama ilivyo India zinajiita mataifa yenye demokrasia kubwa na ya kipekee. Na kinachoonekana ni mataifa hayo kuendelea kulindana na kutetea maslahi yao na hata wakati huu wa vita ya Russia na Ukraine.

Zote zina maslahi sawa ya kuendeleza ubabe kwenye nchi jirani mfano India inadaiwa kulikalia jimbo la Kashmiri lililo mpakani na Pakistani.

Lakini, pia China ina mzozo na Taiwan kadhalika Russia nayo inapambana na Ukraine, ndiyo maana wachambuzi wanaona kuwa wadau hao na washirika muhimu kwenye vita vya sasa na kila mmoja anatetea kila anachoamini kina tija kwake.

China ilikataa kupiga kura kwenye mkutano wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, kuichukulia Russia hatua baada ya kuivamia Ukraine.

### MTIKISIKO KIUCHUMI

Huenda watu wengi wanaweza kudhani kuwa vikwazo vya kiuchumi, kidiplomasia, biashara, utamaduni kama michezo na vya kifedha kama njia ya kuibana Russia imetikisa zaidi nchi hiyo,

INAENDELEA UK. 14

# Dunia shakani, 'samaki mmoja' anavyoumiza tenga la wote



Raia wanashangaa maafa watu kuuawa, majengo na mindombinu kuharibiwa na majeshi ya Russia nchini Ukraine. **PICHA: MTANDAO**

**INATOKA UK. 13**

lakini ukweli ni kwamba labda patakuwa na mtikisiko mkubwa zaidi wa uchumi duniani, ambao haujatokea kwa miaka mingi.

Kwa mfano, Idhaa ya Kiswahili ya DW inasema jambo moja linasalia katika kumbukumbu za Wajerumani ni kutoka kwenye mkutano wa wana habari na Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz na Rais wa Marekani Joseph Biden mwezi uliopita alipoulizwa kuhusu mradi wenye utata wa bomba la gesi la Nord Stream 2, kutoka Russia kuja Ujerumani na Ulaya.

Alikuwa Rais Joe Biden na siyo Scholz, aliyetoa msimamo wa wazi na ahadi kwamba hakutakuwa na bomba endapo Russia itathubutu kutuma wanajeshi nchini Ukraine.

Na hilo ndilo linalotokea leo, Ujerumani inapata wapi nishati, msimu wa baridi unapokaribia?

Ni hatari lakini kuna mengi yameibuka hasa kwenye usalama na hatima ya mataifa ya Ulaya na duniani kwa kuwa Russia ni mshirika wao kila upande.

Katika hatua hiyo ya hatima ya gesi, Ujerumani, inajua ni jinsi gani imeumizwa na vita vya Russia , kwa sababu asilimia 60 ya nishati inatoka Russia, ni balaa , ndiyo maana anayejibu kuhusu suala la bomba la gesi na mafuta kutoka Russia ni Bidden, wangetegemea Kansela Scholz, angejibu.

Russia ni mshirika muhimu kwenye biashara Ulaya, mathalani DW inasema Ujerumani inau-

> Hofu hiyo inaweza kuibuka kutokana na maelezo kuwa yeyote atakayeingilia na kuishambulia Russia atapata kipigo cha kihistoria.



Rais wa Ukraine Volodymyr Oleksandrovych Zelensky, anasubiriwa kufanya maamuzi ya kumaliza au kuendeleza vita yake na Russia. **PICHA: MTANDAO**

za bidhaa nyingi na inategemea masoko ya mauzo yake ya China na Russia, hasa inapokuja kwenye mauzo ya viwanda vikubwa inaiona Russia kama jirani na mtu muhimu kiuchumi.

Shirika la Ndege la Russia maarufu Aeroflot, limepigwa marufuku kuruka kwenye anga la Ulaya, Marekani na dunia nzima inamaanisha kuwa ni hasara kwa mashirika makubwa ya ndege duniani kote iwe Ulaya, Amerika, Japan, Canada, Falme za Kiarabu na Asia.

Abiria na shehena zimekwama na usafirishaji eneo hilo unaacha maswali mengi.

Kibiashara kwa mfano, kampuni ya Japan ya Tumbaku iliyoajiri takribani wafanyakazi 4,500 nchini Russia kuzalisha bidhaa mbalimbali za sigara na kuchangia kiasi kikubwa cha kodi nchini humo hatima yake iko shakani.

Kwa mfano mwaka 2020 ilichangia asilimia 1.4 ya bajeti ya Russia nayo inajiweka pembeni na kuacha pigo kubwa kiuchumi kwa Russia na Japan pia, linasema Shirika la Habari la Uingereza la Reuters.

Kampuni kubwa ya Japan ya MITSUBISHI CORP, linasambaza magari ya Mitsubishi ikiwa na vituo 141 nchini Russia, likiwekeza kwenye miradi ya gesi na mafuta na kupeleka gesi asili ya mitungi Japan, (LNG), uchakataji na uuzaji makaa ya mawe, bidhaa za aluminium, nikeli, pombe ya methanol, plastiki na kusambaza mitambo ya kuzalisha nishati na umeme kwa Russia, yote hayo ni shakani, inaongeza Reuters.

**VITA VYA TATU**

Hofu ya kuwepo vita vya tatu vya nyuklia duniani , huenda isiwe na mashiko kwa sababu juhudi zaidi zinaelekezwa kuibana Russia kiuchumi, kibiashara na kijamii badala ya kupigana vita vya mtutu.

Pengine hakuna kiongozi wala taifa aliye tayari kuona uwekezaji, maisha na hatua zilizofikiwa kimaendeleo leo zikiporomoshwa kwa dakika moja na kuharibiwa na Russia labda kwa kushambuliwa na mabomu ya nyuklia.

Hofu hiyo inaweza kuibuka kutokana na maelezo kuwa yeyote atakayeingilia na kuishambulia Russia atapata kipigo cha kihistoria.

Kwa vile ni taifa lenye makombora ya nyuklia huenda Putin, anaweza kurudia kile kilichofanywa na Marekani nchini Japan kwa kulipua miji ya Nagasaki na Hiroshima mwaka 1945 na mabomu ya atomic na kusababisha maafa yanayoendelea kuwatesa Wajapani hadi leo.





## Rais mgeni rasmi Siku ya Maridhiano

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwenye mgeni rasmi kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Maridhiano yatakayofanyika kitaifa kesho jijini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania, Shekhe Alhad Mussa Salumu, alisema kuwa jumuiya hiyo itakuwa ikitimiza miaka sita tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016 ambapo lengo lilikuwa kushirikiana na serikali katika kuhimiza amani na utulivu kwa Watanzania wote.

"Kauli mbiu ya maadhimisho haya ni, "Tanzania nchi yetu komesha mauaji dumisha upendo, amani na utulivu" imeundwa na viongozi wa dini wa madhehebu mbalimbali hapa nchini bila kujali itikadi ya chama, dini wala kabila lolote."

"Malengo ya Jumuiya ya Maridhiano ni kuleta muafaka katika mambo yanayosababisha tofauti katika dini, mila, siasa na madhehebu mbalimbali ya dini, ikiwamo kusaidia juhudi za serikali katika jitihada zake za kuondoa au kupunguza umasikini, kama ile ya wakulima na wafugaji," alisema.

Aidha, alisema kuwa katika kuelekea kilele hicho wamechangia damu takribani nchi nzima kwa lengo la kuwasaidia watu wenye uhitaji.

"Siku ambayo wana maridhiano wa nchi nzima pamoja na shughuli mbalimbali, pia tumekubaliana kuiathamisha kwa uchangiaji wa damu ili kuokoa maisha ya mama na mtoto, watu waliopata ajali na wagonjwa wengine zoezi ambalo litahitimishwa Machi 3, mwaka 2022, itakayofanyika jijini Dodoma," alisema.

# Utekelezaji agizo la Samia waanza Wizara ya Elimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeanza kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kupanua mafunzo ya ufundi kwa kada ambazo zina uhitaji mkubwa wa wataalamu nchini kwa kujenga vyuo vya ufundi kwenye kanda mbalimbali.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Omary Kipanga, aliyasema hayo alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Dodoma(DIT), kinachojengwa na mkandarasi kutoka kampuni CRJE katika kijiji cha Lugala, jijini hapa kwa gharama ya Sh. bilioni 17.9, kitakachokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,500 kitakapokamilika.

"Baada ya hiki cha Dodoma, tunajenga pia Arusha chuo kikubwa cha mfano wa hiki ambacho pia kitagharimu zaidi ya Sh. bilioni 17, tunajenga Centre of Excellence katika nishati jadidifu, uzalishaji wa umeme kwa kutumia maji, lengo ni kuhakikisha mafundi wa masuala ya uzalishaji wa umeme kwa njia ya maji tunaweza kuwazalisha wenyewe kama nchi," alisema.

Alibainisha kuwa kwa Dar es Salaam kinajengwa kituo kwenye Chuo cha DIT ambapo Sh.bilioni 39 zimepelekwa kwa ajili ya kituo hicho ambapo itakuwa ni kwa ajili ya masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

"Kitakuwa chuo kikubwa kwa ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati lakini ukienda NIT inajengwa Centre of Excellence kwenye masuala ya usafirishaji wa anga na majini, kwa mara ya kwanza katika nchi yetu tutazalisha marubani wetu wenyewe."

"Tuna reli yetu ya mwendo kasi, tunahitaji mafundi waendeshaji wa reli ile, tunakwenda kuzalisha vijana mainjinia kwa ajili watumike kwenye masuala ya anga, bahari na reli ya mwendo kasi, Mwanza tujajenga centre ya masuala ya ngozi, zaidi ya Dola za Marekani milioni 75 tunakwenda kuzitumia kujenga vyuo hivyo," alisema.

Alisema wizara itasimamia ujenzi wa vyuo hivyo kwa kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha kunakuwapo wataalamu wa kutosha katika ulimwengu wa viwanda.

"Serikali yetu imejikita sana kwenye upanuzi wa elimu hii ya kati yaani elimu ya ufundi, kwa hiyo vyuo hivi ni mfano wa vyuo vinavyojengwa katika wilaya, tutajenga kila wilaya nchini Chuo cha VETA, lakini tutajenga kwenye kila mkoa ambapo kwa sasa tunajenga kwenye mikoa isiyokuwa na chuo kabisa ambapo ni Simiyu, Geita, Rukwa na Njombe," alisema.

Pia alisema kwa sasa wanamalizia ujenzi wa vyuo hivyo katika wilaya 25 vingine vimeshakamilika na kuanza kutoa huduma.

"Lengo la serikali ni kushusha elimu ya ufundi katika maeneo yote nchini, na kuhakikisha kwamba Watanzania wanahitaji ujuzi, ufundi wa kutenda zaidi kuliko elimu ile ya nadharia, na mahala pa kuipata ni kwenye vyuo vyetu hivi, nimezunguka nimeona majengo yote tumemwagiza mkandarasi kuhakikisha majengo yote sasa yanakuwa na mafundi muda wote kwasababu mengine tumekuta yamesimama hayana nguvu kazi,"alisema.

Hata hivyo, alisema serikali itahakikisha malipo ya mkandarasi ndani ya wiki hii yanalipwa ili asichelewe utekelezaji wa mradi huo.

"Kazi ilianza Juni 2021 inatarajiwa kukamilika Desemba mwaka huu makusudio yetu kama serikali ifikapo Januari 2023 tuanza udahili hapa, iwapo tukikamilisha mjengo yote chuo kwa awamu ya kwanza kitakuwa na uwezo wa kuweka wanafunzi 600, watakaoishi chuoni, kitakapokamilika kwa ujumla kinatakiwa kuchukua wanafunzi 1,500," alisema.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Mshauri Mwelekezi, Aliki Nziku, alisema utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 38 na kiasi cha Sh. bilioni 3.9 zimelipwa huku akiomba serikali kufikisha miundombinu ya maji na umeme kwa kuwa kwasasa mkandarasi anatumia genereta.

Naye Meneja wa mradi huo, Gao Yuqi, alisema watahakikisha wanatekeleza mradi huo kwa viwango na kwa wakati kulingana na matakwa ya mkataba.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, akizungumza kuhusu mafanikio ya wizara hiyo katika mwaka moja wa utawala wa Rais Samia Suluhu Hassan, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waonywa kuacha ukeketaji mabinti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKAZI wa Mkoa wa Dodoma wametakiwa kuachana na mila za kukeketa watoto wa kike kwa kuwa inasababisha athari mbalimbali wakati wa kujifungua. Kaimu Mganga wa Wilaya ya Chamwino, Dk. Venance Mgaiga, aliyasema hayo katika mkutano wa kujadili Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ulioandaliwa na Shirika lisilokuwa la kiserikali la Women Wake up (WOWAP), uliojumuisha kamati ya ulinzi wa wanawake na watoto ngazi ya halmashauri.

Alisema bado baadhi ya wazazi wamekuwa wakiendeleza kufanya vitendo vya ukeketaji kwa watoto wao, wakidai kwamba vinalinda heshima katika jamii inayowazunguka jambo ambalo si sahihi kiafya.

"Nawaomba wazazi muache tabia hiyo kwa sababu inawaumiza wasichana, ikiwamo kuwaletea athari wakati wa kujifungua," alisema.

Alisema ukeketaji huo umekuwa ukichochea ndoa za utotoni.

Naye Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Chamwino, Janeth Mwakabungu, alisema mara kadhaa wamekuwa wakiwapokea waathirika wa vitendo vya ukatili na kuwapa fomu namba tatu ili kwenda hospitali kupata huduma huku hatua za kisheria zikichukuliwa kwa wahusika.

Kwa upande wake, Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Chamwino, Lucas Kaombwe, alisema kumekuwa kukiibuka mbinu mpya za ukeketaji watoto wakiwa wachanga ili wasijulikane.

Alisema jamii bado inahitaji elimu zaidi ili kupunguza vitendo vya kikatili kwa watoto ambao ni taifa la kesho.

Mratibu wa WOWAP, Nasra Suleiman, alisema lengo la mkutano huo pamoja na mambo mengine lilikuwa ni kuwakumbusha wajumbe wa kamati wajibu wao na kufanya mrejesho wa kazi zilizofanyika. Ofisa Maendeleo Jamii Mkoa wa Dodoma, Honorata Rwegasira, alisema jamii bado inahitaji kupewa elimu kuhusiana na athari za ukeketaji watoto wa kike ili kuondokana na vitendo hivyo.





# Wadau utalii kupatiwa mafunzo ugonjwa Uviko-19

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WADAU 150 wanaohusika katika mnyororo wa sekta ya utalii na ukarimu kwenye mikoa nane nchini, wanatarajiwa kupatiwa mafunzo namna ya kuendesha shughuli zao kupitia mpango wa maendeleo na ustawi wa taifa katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Uviko-19.

Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Utalii, Dk. Shogo Sedoyeka, alitoa kauli hiyo jana alipofungua mafunzo kwa watoa huduma za utalii nchini kuhusu mwongozo wa kukabiliana na ugonjwa wa Uviko-19 katika Sekta ya Utalii.

Alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo wadau wakiwamo mamantilie, wamiliki wa hoteli, waongoza watalii na wafanyabiashara wanajifunza namna ya kukarimu watalii.

Alisema Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kwa kutambua mchango wa sekta ya utalii katika kukuza uchumi wa nchi alitoa fedha kwa ajili ya kuendesha mafunzo kwa wadau wanaohusika na mnyororo wa sekta hiyo ili kuhamasisha utalii.

"Rais Samia Suluhu Hassan mbali na kuzipatia fedha sekta mbalimbali ikiwamo ya elimu, afya, maji na miundombinu, lakini hakuusahau utalii ambapo kupitia fedha za Uviko-19 tumenufaika pia," alisema Dk. Sedoyeka.

Aliitaja mikoa inayonufaika na mafunzo ya watoa huduma katika sekta ya utalii kupewa mwongozo wa kukabiliana na Uviko-19 kuwa ni Mbeya, Iringa, Ruvuma, Mara, Lindi, Mtwara, Njombe na Mwanza.

Katika hatua nyingine Dk. Sedoyeka alisema Chuo cha Taifa Utalii kinaendelea kutoa mafunzo ya utalii na ukarimu kwa wale wote wanaokidhi vigezo vya kujiunga na chuo hicho ili kujifunza namna bora ya kutangaza vivutio mbalimbali hapa nchini.

Akifungua mafunzo hayo, kwa niaba ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Salum Manyatta, alisema ugonjwa wa corona ulichangia kwa kiasi kikubwa kupunguza idadi ya watalii nchini.

Alisema mwaka 2019 Tanzania ilipokea watalii milioni 1.5 na baada ya kuripotiwa janga la corona mwaka 2020 idadi ilishuka hadi watalii 602,800.

Pia, alisema licha ya kikwazo cha ugonjwa wa corona, lakini serikali inaendelea na jitihada mbalimbali katika kukuza utalii kwa kuhakikisha watoa huduma wanapata chanjo pamoja na kuweka miundombinu rafiki ya kukabiliana na ugonjwa huo ili kujilinda na kuwalinda wageni.

Alisema katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi wamepanga kuwafikia watalii milioni tano ifikapo mwaka 2025 na kwamba wataendelea kuvitangaza vivutio mbalimbali kwa kutumia vyombo vya habari.

Miongoni mwa washiriki wa mafunzo hayo jijini Mbeya, Nafisa Mtoro, alisema suala la ukarimu kwake lilikuwa tatizo na baada ya kupewa elimu ya namna bora ya kukaribisha wateja itamsaidia kufanya biashara yake ya chakula na kujiingizia kipato.



Mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, akizungumza na wadau wa utalii wa mkoa huo, wakati wa mafunzo kwa watoa huduma za utalii nchini kuhusu mwongozo wa kukabiliana na ugonjwa wa Uviko-19 jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mbunge CHADEMA afunguka kura zao kwa Dk. Tulia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Sophia Mwakagenda, amesema wabunge wanaotokana na chama hicho waliamua kumpa kura ya ndiyo Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson baada ya kuridhishwa na utendaji kazi wake.

Mwakagenda alitoa kauli hiyo juzi wakati wa tafrija ya kumpongeza Dk. Tulia baada ya kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Tanzania iliyofanyika jimboni kwake Mbeya Mjini.

Alisema utendaji kazi wa Dk. Tulia uliwashawishi wabunge hao kumpigia kura ili awe Spika wa Bunge na kuwaongoza kwa weledi wa hali ya juu.

"Sisi wabunge wa CHADEMA tulimpigia kura ya ndiyo, Dk. Tulia ili awe spika kwa wabunge kwa sababu ya utendaji kazi na utashi katika kuongoza vikao vya Bunge, lakini pia ni mwanamke mwenzetu ilikuwa lazima tumpigie kura," alisema Mwakagenda.

Aidha, alisema wabunge wa CHADEMA wataendelea kumuunga mkono Spika Dk. Tulia kwa manufaa mapana ya taifa katika kuwaletea maendeleo wananchi kupitia mijadala na hoja mbalimbali ambazo zitakuwa zinawasilishwa bungeni.

Katika hafla hiyo Spika wa Bunge, Dk. Tulia aliwaahidi Wanambeya kuwatumikia kwa kuhakikisha maendeleo yanapatikana ikiwamo ujenzi wa barabara ya njia nne kutoka mjini Igawa hadi boda ya Tunduma iliyoko mkoani Songwe.

Alisema hadi kufika Julai, mwaka huu mkandarasi atakayehusika na usanifu atakuwa amepatikana tayari kwa ajili ya kuanza shughuli ya usanifu.

Kwa upande wake, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, Marry Mwanjelwa, amempongeza Dk. Tulia kuwa Spika na kumwombea mema katika utekelezaji wa majukumu yake na kumsihi asiogope Mungu atamsimamia.

## N/waziri asisitiza wananchi kutunza vyanzo vya maji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, amezindua upandaji miti katika Mtaa wa Mayombo, Kata ya Iwambi na kusisitiza wananchi kutunza vyanzo vya maji ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Mahundi alitoa kauli hiyo juzi alipozindua upandaji miti ulioandaliwa na kikundi cha Active Group chini ya mwenyekiti wa kikundi hicho, Melania Kifaru.

Alisema miti 2,200 imepandwa kwenye taasisi za umma ikiwamo shule, zahanati na ofisi za mtaa pamoja na wananchi kukabidhiwa miti mitatu ya matunda na vivuli kwa ajili ya kutunza mazingira.

"Nawapongeza wanakikundi kwa kutambua umuhimu wa kutunza uoto wa asili ili vyanzo vya maji visikauke na huduma zipatikane kwa uhakika hususani nyakati za kiangazi," alisema Mhandisi Mahundi.

Akizungumza wakati wa upandaji miti, Mwalimu wa Shule ya Msingi Iwambi, Elia Kasanga, alisema miti katika shule hiyo itasaidia kuvutia mazingira na hali ya hewa kuwa safi.

Alisema pia waliwaomba wadau kuwasaidia vitendea kazi ikiwamo kompyuta ili kurahisisha utendaji kazi shuleni hapo.

Akizungumza kwa niaba ya Diwani wa Kata ya Sinde, Fanuel Kyanula, alisema upandaji miti jijini Mbeya umeendelea kuungwa mkono na wadau mbalimbali wakishirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari), Kituo cha Uyole kuwapatia wananchi miche ya aina mbalimbali ikiwamo matunda na vivuli.

Alisema kwa sasa kupitia vikao vya madiwani wamepanga kuhamasisha wananchi kupanda miti ya aina mbalimbali kuzunguka maeneo yao ili kupata faida ikiwamo matunda.



## HABARI ZANZIBAR

# ZECO kununua nguzo za umeme toka Iringa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini, Suleiman Masoud Makame, amesema Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) sasa litanunua nguzo za umeme kutoka Iringa badala ya nje ya nchi.

Makame alisema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi na kujibu swali la Mwakilishi wa Mfenesini, Machano Othman Said, aliyetaka kujua kwa nini shirika limeshindwa kutoa nguzo za kusambaza umeme kwa wananchi vijijini.

Alisema awali ZECO ilikuwa ikinunua nguzo za umeme kutoka nje ya nchi lakini kutokana na kuibuka kwa changamoto mbalimbali, likiwamo tatizo la usafiri, limelazimika kununua nguzo hizo kutoka Iringa.

"Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba hivi sasa tunanunua nguzo za kusambaza umeme kutoka Iringa, Tanzania Bara. Awali ilikuwa tunanunua nje ya nchi lakini kutokana na tatizo la usafiri sasa tumebadilisha mwelekeo," alisema.

Pia alisema shirika linatarajia kusambaza umeme katika vijiji 61 Unguja na Pemba hatua ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kufikisha huduma hiyo majumbani.

Alisema kwa kutumia nguzo za kusambaza umeme zilizopo, sasa linatarajia kuifanya kazi hiyo kwa ufanisi na hadi kufikia mwezi huu, tayari wananchi wamepata huduma hizo.

**Pia alisema shirika linatarajia kusambaza umeme katika vijiji 61 Unguja na Pemba hatua ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kufikisha huduma hiyo majumbani.**

# Zanzibar yapata bil. 4.4/- mgawo tozo miamala ya simu kwa miezi 3

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Jamal Kassim Ali, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepata mgawo wa Sh. 4,432,693,692 ikiwa ni kodi za miamala ya simu kwa Julai hadi Septemba, 2021.

Jamal aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mpendae, Shaaban Ali Othman, aliyetaka kujua kiwango cha fedha za kodi za miamala ya simu pamoja na zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi gani ya maendeleo.

Alisema fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa shule, hospitali ambayo mahitaji yake yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku.

Kutokana na kuwapo kwa msongamano mkubwa wa wanafunzi katika shule za Unguja na Pemba, alisema serikali imejipanga kuzitumia fedha hizo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa shule zikiwamo za ghorofa.

"Fedha za miamala ya kodi za simu tumejipanga kuzielekeza katika ujenzi wa shule za msingi na sekondari kwa ajili ya kupunguza msongamano wa wanafunzi shuleni," alisema.

Pia alisema fedha zingine zitaelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa hospitali zikiwamo zinazotoa huduma za wajawazito na watoto zikiwamo za vijijini.

Alisema serikali imejipanga kumaliza tatizo hilo ikiwa ni sehemu ya mikakati ya dira ya maendeleo 2050 kuona vifo vinavyotokana na wajawazito na watoto vinatokomezwa moja kwa moja.

"Mgawo wa fedha zinazotokana na tozo za simu tumejipanga kuzielekeza moja kwa moja katika kuimarisha sekta ya afya ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya kwa ajili ya wajawazito na watoto hadi vijijini Unguja na Pemba," alisisitiza.



Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wakifuatilia kikao cha baraza hilo, kinachoendelea Chukwani, nje ya Mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali kukarabati vituo 168 vya afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya, Ustawi Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto imesema imejipanga kuvifanyia ukarabati mkubwa vituo vya afya 168 Unguja na Pemba vikiwamo vilivyoko vijijini.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui, alipokuwa akijibu swali la Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamad Omar, aliyetaka kujua lini Kituo cha Afya kisiwani humo kitafanyiwa ukarabati na kupatiwa madaktari na wauguzi wa kutosha.

Mazrui alisema wizara imejipanga kuona vituo vya afya vilivyoko katika visiwa vidogo kikiwamo cha Kojani vinafanyiwa matengenezo makubwa na kupatiwa madaktari na wauguzi.

Alisema juhudi hizo zimechukuliwa kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanaoishi katika visiwa vidogo wanapata huduma zote za muhimu ambazo ni matibabu na elimu.

Waziri alisema tayari serikali imetoa kibali cha ajira kwa sekta ya afya na kwamba vituo vya afya vilivyoko vijijini vitapata madaktari wa kutosha na wafanyakazi wake.

"Mheshimiwa Naibu Spika nataka niwatoe wasiwasi wananchi wanaoishi katika visiwa vidogo vidogo Unguja na Pemba kwamba serikali tumejipanga kufikisha huduma hizo hatua ambayo itawapunguzia safari wananchi kwenda upande wa pili ikiwamo kuvuka bahari," alisema.

Mazrui pia alisema kwa upande wa kisiwa cha Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja, wizara imejipanga kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya chenye huduma za wajawazito na watoto.

Waziri Mazrui alikiri kuwa kituo hicho kinakabiliwa na ukosefu wa madaktari na wauguzi mbalimbali na hiyo inatokana na wafanyakazi wanaoajiri wakiwamo wanawake huamba ajira mara wanapoolewa.

"Wizara ya Afya imejipanga kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya cha Tumbatu ingawa pia tumewasiliana na mfadhili mmoja ambaye ameahidi kujenga hospitali kubwa ambayo itawafanya wananchi wa kisiwa hicho kuacha kuvuka bahari kwenda katika hospitali nyingine ikiwamo ya Mkokotoni," alisema.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO

NYUMBA INAUZWA KIJITONYAMA MAKUMBUSHO KARIBU NA KITUO CHA MABASI.

WASILIANA NA 0654251570 AU 0686096001

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MBEYA**
**SHAUR LA MADA NA.75/2021**
**INNOCENT NSEGIYUMUA ……………MDAI**
**DHIDI YA**
**BENARD JUBECK MWAKAMBOJA…..MDAIWA**
**KWA;**
**BENARD JUBECK MWAKAMBOJA**
**POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

Unataarifiwa na mahakama hii kuhudhuria hapa mahakama ya wilaya mbeya au wakili wako mnamo tarehe 04/03/2022 siku ya Ijumaa saa 3:00 asubuhi, ambapo shaurilimepangwa kusikilizwa.

**ELEWA KWAMBA.** Ukikosa kufika siku hiyo shauri hili litasomwa bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 22 mwezi 02 mwaka 2022.

HAKIMU MKAZI
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA WILAYA MBEYA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya**
**Wilaya ya ………...TANGA**
**Kituo cha….. MJINI TANGA…. Mkoa… TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi…………44…………2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: HAJIRA JOHN MWINAMI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA**
**NA: STELLA JOHN MWINAMI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslai yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21/3/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo 28/02/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu RAMADHAN HALFAN SWAGO anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya HYUNDAI BAKKIE yenye namba za usajili T 324 DDZ. Yenye Chassis No: MMFZBX7BL04956385 Na. Engine No: 55888888 Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: TAN/RB/65374/2022

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya Wilaya ………TANGA………**
**Kituo cha …..MJINI….TANGA…..Mkoa……TANGA……**
**Shauri la Madai Na……38…………..2022…………**
**Jina la mdai …MKURUGENZI SONI AUTO AND LABS SUPPLIES COMPANY LTD**
**Jina la Mdaiwa…MKURUGENZI KILIMANJARO CEMENT COMPANY LTD**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa ….MKURUGENZI KILIMANJARO CEMENT COMPANY LTD WA PONGWE**

Kwa kuwa Mdai ameleta Madai yake kwamba anakudai TSHS 14,695,132/=
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii 4/03/2022 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo 24/2/2022.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NDUGU MAULID JOHN MAULID** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** yenye namba za usajili **MC 739CGG.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/24737/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI GARI

**MACHA HASANI LASWAI** Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye namba usajili **T 564 BNG** yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0784519167 au 0652066959 DSM/PHQ /RB/502412/2022**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **THEONESTINA KAGEMULO ABEL** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya Mitsubish Canter lenye namba za usajili **T434CWM,** Injini namba **4D33EAA2972** na Chassis namba **FE517BD402972.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/83793/2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye au apige simu namba **0753654951.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Ndugu THEONESTINA KAGEMULO ABEL** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya Nissan Datsan lenye namba za usajili **T706 BSJ,** Injini namba **NA16009678N** na Chassis namba **GD21429206.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/83725/2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye au apige simu namba **0753654951.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**EVODIA EMMANUEL RUSAGARA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3623-0017** cha **ST. VINCENT DE PAUL SEKONDARI** mwaka **2012.** Living Certificate ya Chuo cha **TEOFILO KISANJI** Reg. namba **TEKU/CAF/013/314** mwaka **2013/2014.** Academic Transcript ya **TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY** Reg. namba **MZA/DA/14/24182** mwaka **2015/2016.** Cheti cha kuzaliwa namba **337/2014.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/83923/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SAIDI RASHIDI HEMEDI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SUZUKI CARRY** yenye namba za usajili **T 145 CZU**, Engine Na. **F6AEAA1693,**Chassis Na.**DD51T301693** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **TAN/RB/69575/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **TWAHIRU ABEDI SHUI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **CRUISER** yenye namba za usajili **MC 630 BEQ** Yenye Chassis No: **LP6LCJD0790CR0006** Na. Engine No: **156FM195101600** Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: **TAN/RB/20742/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABDULRAHMAN ABDI ABASI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya GARI VOLVO yenye usajili namba **T 649 CBP,** Engine **Na.0000282489,** Chassis Na.**YV2A4CECX2A547423.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **TAN/RB/66322/2022.**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE

# Msafara wa jeshi Russia waikaribia Kyiv, mazungumzo yaingia siku ya 2

**Kyiv,** UKRAINE

WAKATI mashambulizi ya Russia kijeshi dhidi ya Ukraine, ikiwa ni wiki moja leo, msafara wa magari ya Jeshi la Russia wenye urefu wa kilomita 64, umeonekana ukielekea mji mkuu, Kyiv, licha ya mazungumzo kutuliza hali ya ghasia katika mpaka wa Ukraine-Belarus kuingia siku ya pili.

Msafara huo umeonekana kwa njia ya picha ya satelaiti, vyombo vya habari mbalimbali vya kimataifa viliripoti.

Inakadiriwa Russia, imeongeza idadi ya wanajeshi wake nchini Ukraine kutoka asilimia 40 hadi karibu 75, kwa mujibu wa ofisa mkuu wa ulinzi wa Marekani.

Msafara huo, umetajwa kuongeza hofu na idadi ya watu kuhama Ukraine na wengine kuendelea kujichimbia kwenye makazi ya ardhini na vituo vya treni.

Pia inaelezwa Russia, inazingira maeneo yenye watu wengi kwa kutumia mbinu za enzi za kati, wakilenga maeneo wanayoyazunguka kuwanyima chakula, maji na vifaa muhimu.

Wakati uvamizi huo ulipoanza, kulikuwa na matarajio kwamba ingekuwa ni suala la siku moja, hata la saa kadhaa kabla ya jeshi kubwa la Russia kuingia Kyiv.

Jeshi la Russia limekutana na upinzani uliowekwa na jeshi la Ukraine, kwa kutumia silaha na risasi za msaada kutoka nchi za Magharibi, pia inalindwa na wananchi ambao wanachukua bunduki, kusaini kwa vikosi vya ulinzi vya jirani na kwenda hadi mistari ya mbele.

Lakini hakuna ubishi kwamba msafara huu, hata kama unazidi kukaribia na milipuko inazidi kukaribia.

Walikuwa hasa kwenye ukingo wa jiji, jana usiku palikuwa karibu sana hivi kwamba jengo letu wenyewe lilitikisika.

#### MJI KHARKIV WASHAMBULIWA

Mji wa Kharkiv ambao ni wa pili kwa ukubwa, umekumbwa na shambulio la Russia. Shambulio hilo la jana asubuhi lilionekana kulenga ofisi za serikali katika eneo la Freedom Square katikati mwa jiji.

Maofisa wa dharura wa eneo hilo waliandika kwenye mtandao wa Facebook kwamba raia sita walijeruhiwa wakati wa shambulio la makombora katika ofisi ya utawala wa serikali, akiwamo mtoto mmoja.

Makombora ya Russia yamegonga kitovu cha kitamaduni cha mji wa pili wa Ukraine katika kile maofisa walisema ni shambulio baya.

Jumba la opera, ukumbi wa tamasha na ofisi za serikali zilipigwa katika Freedom Square, katikati mwa jiji la Kaskazini-Mashariki, Kharkiv. Takriban watu 20, ikiwamo na mtoto walijeruhiwa, ingawa mamlaka bado wanajaribu kubaini kama mtu yeyote aliuawa.

Shambulio hilo limetokea huku Rais wa Ukraine akisema Urusi ilikuwa ikifanya uhalifu wa kivita.

"Hivi ndivyo asubuhi yetu inavyoonekana, watu wa Ukraine," Rais Volodymyr Zelensky alisema. "Huu ni ugaidi dhidi ya Ukraine.

Hakukuwa na malengo ya kijeshi katika uwanja huo - wala hawako katika maeneo ya makazi ya Kharkiv ambayo yanapigwa na makombora," aliongeza.



Jengo la Utawala Mkoa wa Kharkiv, lilikuwa kati ya majengo yaliyoshambuliwa jana. Inakadiriwa raia 350 wamepoteza maisha, ikiwa ni takribani wiki moja tangu mashambulizi ya Russia dhidi ya Ukraine, yaanze. **PICHA: AP**

**Wakati USSR ilipoweka makombora yenye silaha za nyuklia nchini Cuba mwaka 1962, nchi za Magharibi zilikuwa tayari kulipua ulimwengu juu yake. Sasa NATO ikifanya hivyo wanatarajia Urusi kufanya tofauti.**



Mbunge wa Bunge la Ukraine, Sviatoslav Yurash (26), akiwa na silaha mjini Kyiv. **PICHA: ALJAZEERA**

Picha za video zilionyesha kombora likipiga jengo la serikali ya mtaa na kulipuka, na kusababisha moto mkubwa. Kharkiv imekuwa ikishambuliwa kwa mabomu kwa siku kadhaa sasa.

Serikali ya Ukraine inaishutumu Russia, kwa kujaribu kuizingira Kharkiv na miji mingine, ukiwamo mji mkuu wa Kyiv, ambako msafara mkubwa wa kivita wa Urusi unakaribia.

#### MTOTO MUSEVENI AUNGA MKONO

Mtoto mwenye nguvu kiutawala wa Rais wa Uganda Yoweri Museveni, Luteni Jenerali Muhoozi Kainerugaba, ameelezea kuunga mkono uvamizi wa Urusi nchini Ukraine.

Jenerali Kainerugaba, ambaye ni kamanda wa majeshi ya nchi kavu ya Uganda, aliweka ujumbe kwenye mtandao wa Twitter, kwamba "binadamu wengi (ambao si wazungu) wanaunga mkono msimamo wa Urusi nchini Ukraine".

"Putin yuko sahihi kabisa!" aliongeza.

"Wakati USSR ilipoweka makombora yenye silaha za nyuklia nchini Cuba mwaka 1962, nchi za Magharibi zilikuwa tayari kulipua ulimwengu juu yake. Sasa NATO ikifanya hivyo wanatarajia Urusi kufanya tofauti."

Jenerali Kainerugaba ndiye ofisa mkuu wa kwanza wa kijeshi barani Afrika kuunga mkono hadharani uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

Inasemekana kuwa anaweza kuwa mrithi wa babake mwenye umri wa miaka 77, ambaye amekuwa madarakani tangu 1986.

Umoja wa Kanda ya Afrika Magharibi ECOWAS umelaani uvamizi wa Russia, huku Umoja wa Afrika (AU) ukiitaka Moscow kuheshimu 'eneo la uadilifu'. Wizara ya Mambo ya Nje ya Afrika Kusini imetoa wito wa kuondolewa kwa wanajeshi wa Urusi kutoka Ukraine.

Jenerali Kainerugaba pia alituma tena ujumbe wa mwanahabari mashuhuri wa Uganda Andrew Mwenda, ambaye alisema kwamba hata "mgeni katika siasa za kimataifa anaweza kuona kwamba Moscow haiwezi kamwe kuruhusu Ukraine kujitosa kwa NATO, EU, kwa sababu inaleta tishio kwa Russia.

**Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao**

# COASTAL YAMPIGA CHINI KOCHA SIMBA KURITHI MIKOBA YA MEDO

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa zamani wa Simba Goran Kopunovic, ni miongoni mwa makocha walioomba kazi ya kuifundisha Klabu ya Coastal Union ya Tanga ambayo kwa sasa ipo chini ya Kocha Msaidizi, Joseph Lazaro, baada ya kuachana na Kocha Melis Medo.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Rashid Mgweno, amesema pamoja na Mserbia huyo aliyeifundisha Simba kwa kipindi kifupi mwaka 2015 na kuipa ubingwa na Kombe la Mapinduzi, hakuweza kufanikiwa kupita kwenye mchujo, huku akikanusha taarifa za aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu ya Taifa, Taifa Stars, Azam FC na Mbao, Ettiene Ndayiragije kuwa ndiye atakayechukuwa kikosi hicho.

Katika hali ya kushangaza, amesema hakukuwa na ombi lolote kwa makocha wa Kitanzania, hivyo Kocha Mkuu wa Coastal Union atakuwa ni wa kigeni.

"Tulikuwa na majina mengi ya makocha mbalimbali kutoka nje ya nchi na hatukuwa na kocha yeyote Mtanzania aliyeomba, hilo lieleweke wazi. Makocha kutoka nje ya nchi akiwamo kocha wa zamani wa Simba Goran (Kopunovic) ambaye ni Mserbia naye aliomba, lakini hakufanikiwa kupenya kwenye mchujo, kwa sasa tumebakisha majina ya makocha watatu, wawili ni Warundi na mmoja ni Mnyarwanda," alisema Mgweno na kuongeza. "Wengi wanadhani ni Ndayiragije, lakini hawa watatu waliopenya kwenye mchujo na tunarajia kumtangaza mmoja wapo siku yoyote, hawajawahi kufundisha klabu yoyote nchini. Mmoja amewahi kuifundisha Vital'O ya Burundi na mwingine Bandari ya Kenya," alisema Katibu huyo.

Alisema kazi ya mchujo, kuangalia CV (wasifu), zinazoendana na vigezo vilivyowekwa na Shirikisho la Soka nchini (TFF), inaongozwa na mchezaji na kocha wa zamani wa timu hiyo, Juma Mgunda.

Coastal iliachana na Medo baada ya timu hiyo kufanya vibaya kwenye mechi zake za Ligi Kuu.

**TUNAWEZA...**



Afisa Mkuu Raslimali Watu Benki ya NMB, Emmanuel Akonaay (mwenye jezi nyeupe) pamoja na Meneja Kanda ya Ziwa, Baraka Ladislaus, wakishiriki mbio za Kilomita 21 za Kilimanjaro Marathon 2022 zilizofanyika mjini Moshi mwishoni mwa wiki. Benki hiyo kupitia klabu yake ya 'NMB Jogging' ilishiriki kikamilifu kwenye mbio za Kilomita tano, 21 na 42. **MPIGAPICHA WETU**

# *Shabiki Simba ashinda milioni 176/- M-BET*

**Na Mwandishi Wetu**

SHABIKI wa Klabu ya Simba na Arsenal, Swalehe Enzi, ameshinda kitita cha Sh. 176,470,910 kupitia mchezo wa kubashiri wa Perfect 12 wa Kampuni ya M-Bet Tanzania.

Enzi ambaye ni mkazi wa Mtwara, ameshinda kiasi hicho kikubwa cha fedha baada ya kubashiriki kwa usahihi matokeo ya mechi 12 za soka za ligi mbalimbali duniani kwa kutumia Sh. 1,000 tu.

Alisema kuwa alibashiri kwa kipindi cha miaka mitatu huku akishinda kiasi cha fedha kidogokidogo ambazo hazikumkatisha tamaa.

Enzi alisema pamoja na yeye kuwa shabiki wa Simba na Arsenal, bado huwa anakumbana na vipingamizi vingi katika kubashiri kwake jambo ambalo limekuwa likimwaribia 'mkeka' wake na 'kuchanika'. "Mimi ni fundi seremala na nimekuwa nikibashiri kwa kutumia madaftari (madogo) ama 'counterbook'. Nimefanya hivyo kwa miaka mitatu huku nikishinda zawadi za fedha ndogondogo.

"Sikuweza kukata tamaa kwani nimeshuhudia washindi kadhaa kupitia Perfect 12 ya M-BET wakishinda mamilioni. Nilijua ipo siku nami nitashinda kwani hakuna ubabaishaji, natoa wito kwa vijana wenye umri kuanzia miaka 18, kubashiri kupitia M-BET," alisema Enzi.

Alisema hakuamini alipopigiwa simu kuwa ameshinda kiasi hicho kikubwa cha fedha na kwamba sasa mipango yake ni kuendeleza biashara na kuanzisha nyingine, kusomesha na kujenga nyumba.

Kwa upande wa Meneja Masoko wa M-BET Tanzania, Allen Mushi, alisema kuwa wanajisikia fahari kubwa kubadilisha maisha ya Watanzania kupitia michezo yao.

Mushi alisema Watanzania wengi wamekuwa wakibashiri na kushinda kupitia michezo yao na kufanikiwa kupiga hatua kubwa za kimaendeleo.

"Huu ni mwanzo wa mwaka na tayari washindi wamepatikana, tutaendelea kuwa nyumba za washindi na kubadili maisha ya Watanzania," alisema Mushi.

# Polisi yaiandalia 'kwata' Azam FC

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Polisi Tanzania umesema baada ya kupoteza mchezo uliopita dhidi ya timu ya KMC, sasa unaendelea kutafuta mbinu za kuifumua Azam FC kwenye mechi watakayocheza Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Robert Munisi, alisema Kocha wao mkuu, Malale Hamsini, anaendelea kuyafanyia kazi makosa aliyoyaona kwenye mchezo uliopita.

"Kikosi kinaendelea kujiweka sawa kwa ajili ya kujiandaa kukutana na Azam hapo Jumamosi," alisema Munisi.

Mwenyekiti huyo, alisema lengo lao ni kupata pointi tatu kwenye mchezo huo ambao amekiri kwamba utakuwa na ushindani mkubwa.

Aliweka wazi kuwa Ligi Kuu ya NBC msimu huu ina ushindani mkubwa, hivyo wanajipanga kuhakikisha kila mechi wanapata matokeo mazuri na kudai kila mchezo wanauchukulia kama fainali.

Naye Afisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Juma, alisema wamejipanga kuvuna alama tatu kwenye mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa mgumu, hivyo akawataka mashabiki wasahau matokeo waliyoyapata kwenye mchezo uliopita na badala yake waendeleze ushirikiano wao kwa wachezaji.

"Kocha wetu Malale Hamsini anaendelea kufanyia kazi makosa madogo aliyoyabaini kwenye mchezo uliopita huku akiendelea kuwajenga kisaikolojia wachezaji," alisema Juma.

## ZISIKUPITE

### SAKA HAONDOKI ARSENAL

WINGA wa England, Bukayo Saka ana furaha Arsenal licha ya ripoti kueleza kuwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 20, amesimamisha mazungumzo ya kuongeza mkataba wake mpya. ***(Fabrizio Romano)***

### PALHINHA ATAKIWA UNITED

MANCHESTER United imeonyesha pia nia ya kumtaka kiungo wa Sporting Lisbon, Joao Palhinha. (***Record, via Sun)***

### MESSI SASA ANUKIA MLS

KLABU ya David Beckham inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani (MLS), Inter Miami itafanya kila linalowezekana kumsajili Lionel Messi mwenye umri wa miaka 34, iwapo mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina ataamua kuondoka Paris St-Germain mapema msimu huu. ***(Miami Herald, via Mail***)

### MADRID YAKOMAA NA MBAPPE

KLABU ya Real Madrid inatarajia kwanza kukamilisha mpango wa kumsajili mshambuliaji Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23, kutoka PSG kabla ya kuanza usajili wachezaji wengine au kuwaongezea mikataba wachezaji waliopo. ***(Goal***)

### DAVID KUONDOKA LILLE

NYOTA anayesakwa na Arsenal, Jonathan David mwenye umri wa miaka 22, ana mpango wa kuondoka Lille msimu huu. (***Sky Germany, via Express***)

### JUVE YAONGOZA KWA ZANIOLO

JUVENTUS inaongoza mbio za kumuania winga wa Italia, Nicolo Zaniolo mwenye umri wa miaka 22, ambaye bado hajasaini mkataba mpya na klabu yake ya AS Roma***. (Luca Bianchin via SB Nation)***

### YATES AWINDWA NOTTINGHAM

KLABU ya Nottingham Forest imeanza mazungumzo na kiungo, Ryan Yates mwenye umri wa miaka 24, ikipambana pia kumbakiza kiungo anayesakwa sana raia wa Wales, Brennan Johnson mwenye umri wa miaka 20 ambaye anahusishwa na Tottenham. (***Mirror***)

### RAMOS ANYATIWA GALAXY

KLABU ya LA Galaxy inavutiwa kumsajili mlinzi wa kati, Sergio Ramos mwenye umri wa miaka 35, ambaye anahaha kuonyesha cheche zake kule Paris St-Germain kwa sababu ya majeraha yanayomuandama. ***(Foot Mercato)***

### CRUYFF ATAJWA AJAX

AJAX inataka kumteua mshauri wa michezo wa Barcelona, Jordi Cruyff kuwa mkuregenzi wao mpya wa soka baada ya kuondoka kwa Marc Overmars. (***Marca***)

### OSIMHEN AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inajiandaa kulipa kitita cha pauni milioni 100 kumsajili mshambuliaji Mnigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 23 kutoka Napoli. ***(Star***)

### MORATA YUPO SANA JUVE

KLABU ya Juventus pia ina matumaini ya kumbakiza mshambuliaji, Alvaro Morata mwenye umri wa miaka 29. (***Gazzetta dello Sport***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LAPORTA: DEMBELE ATABAKI BARCELONA

**Anajua ofa yetu na kwamba tumekuwa tukimtaka abaki, tunatumaini kwamba mwisho wa msimu ataifikiria tena...**

**BARCELONA,** HISPANIA

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta anatumaini, Ousmane Dembele atabadilisha msimamo wake na kutafakari upya ofa ya mkataba mpya kutoka kwa klabu hiyo ya Katalunya.

Dembele ameshindwa kuafiki kuongezwa kwa mkataba wake wa sasa unaotarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, hakufanikiwa kuondoka Barca Januari na kocha mkuu Xavi amekuwa akimtumia kwenye mechi zake.

**Dembele alicheza vizuri Jumapili dhidi ya Athletic Bilbao, akifunga bao moja na kusaidia mengine mawili wakati Barca ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0.**

Hilo lilimfanya kuwa mchezaji wa kwanza wa akiba wa 'Blaugrana' hao kuchangia mabao matatu katika mchezo mmoja wa LaLiga karne hii, na Laporta alieleza matumaini yake kwamba mchezaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund bado anaweza kubaki.

"Dembele anajua ofa yetu na kwamba tumekuwa tukimtaka abaki. Tunatumaini kwamba mwisho wa msimu ataifikiria tena," alisema Laporta akinukuliwa na Cadena Sere.

Wakati Dembele aking'ara dhidi ya Athletic, Xavi naye alitoa sifa maalum baada ya mchezo huo kwa Pedri, ambaye alimfananisha na mchezaji mwenzake wa zamani, Andres Iniesta.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 985

MECHI KALI
TANZANIA PRISONS
VERSUS
MTIBWA SUGAR
1 | 4.00
X | 2.90
2 | 2.14

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# FIFA NA UEFA ZAIFUNGIA URUSI




**NYON,** Uswisi

SHIRIKISHO la Soka la Kimataifa, (FIFA), na lile la Ulaya (UEFA), zimepiga marufuku timu za Urusi kushiriki mashindano ya klabu na kimataifa, na kuwanyima kushiriki Kombe la Dunia la mwaka 2022 na michuano ya Euro 2022 ya Wanawake.

Uamuzi huo unamaanisha kuwa Klabu ya Spartak Moscow itaondolewa kwenye hatua ya 16-bora ya Ligi ya Europa, ambapo walipaswa kuvaana na RB Leipzig.

UEFA pia imemaliza uhusiano wake na Gazprom, kampuni kubwa ya nishati inayomilikiwa na Serikali ya Urusi ambayo ilikuwa Mfadhili Mkuu wa Ligi ya Mabingwa Ulaya. Taarifa ya pamoja ya FIFA na UEFA ilisema: "Kandanda imeunganishwa kikamilifu hapa na katika mshikamano kamili na watu wote walioathiriwa nchini Ukraine.

"Marais wote wawili (Gianni Infantino na Aleksander Ceferin) wanatumaini kuwa hali nchini Ukraine itaimarika kwa kiasi kikubwa na kwa haraka ili mpira wa miguu uweze tena kuwa chanzo cha umoja na amani miongoni mwa watu."

Ulimwengu wa michezo umetoa wito wa kuwekewa vikwazo Urusi kufuatia uvamizi wa Rais Vladimir Putin nchini Ukraine wiki iliyopita.

Poland, Sweden na Jamhuri ya Czech - wapinzani wa Russia katika hatua ya mtoano ya Kombe la Dunia - zote zilitangaza kugomea mechi zao, ingawa vikwazo vya awali vya FIFA viliruhusu Shirikisho la Soka la Urusi kuweka mbele timu inayocheza kwa jina tofauti na bendera katika eneo lisilo na upande.




# Pele apona sasa atoka hospitali

**SAO PAULO,** Brazil

GWIJI wa soka wa Brazil, Pele ameruhusiwa kutoka hospitalini baada ya kutibiwa maambukizi ya mfumo wa mkojo.

Pele alilazwa katika Hospitali ya Albert Einstein jijini Sao Paulo Februari 13, mwaka huu kwa matibabu ya uvimbe wa utumbo mpana.

Madaktari waligundua maambukizi kwenye mfumo wa mkojo (UTI) siku nane baada ya kulazwa, lakini wakasema Jumatatu kuwa suala hilo limetatuliwa.

Taarifa kutoka hospitali ilisema: "Hali za kliniki za mgonjwa ziko sawa na amepona maambukizi yake.

"Ataendelea na matibabu ya ya uvimbe wa utumbo mpa uliotambuliwa Septemba 2021."

Pele mwenye umri wa miaka alilazwa tena hospitalini kwa ma babu ya uvimbe wake Desemba mwaka jana kabla ya kuruhusi Desemba 23.

Mshindi huyo mara tatu Kombe la Dunia, ni mmoja wa chezaji wanne pekee waliofun katika michuano hiyo minne fauti.

Anabakia kuwa mfungaji bo wa muda wote wa Brazil aki amefunga mabao 77 katika mic zo 92, mabao saba mbele ya ny wa Paris Saint-Germain, Neym (70).

,669,400

# JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/03/22 | 18:00 | Wolverhampton vs Crystal Palace | 2.29 | 3.09 | 3.34 |
| 02. 05/03/22 | 18:00 | Newcastle vs Brighton | 2.70 | 3.14 | 2.70 |
| 03. 05/03/22 | 18:00 | Aston Villa vs Southampton | 2.30 | 3.36 | 3.06 |
| 04. 05/03/22 | 18:00 | Norwich City vs Brentford | 2.95 | 3.10 | 2.50 |
| 05. 05/03/22 | 20:00 | Roma vs Atalanta | 2.41 | 3.40 | 2.85 |
| 06. 06/03/22 | 14:30 | Genoa vs Empoli | 2.61 | 3.26 | 2.71 |
| 07. 06/03/22 | 16:00 | Cadiz CF vs Rayo Vallecano | 3.31 | 3.06 | 2.32 |
| 08. 06/03/22 | 17:00 | Reims vs Strasbourg | 3.48 | 2.78 | 2.39 |
| 09. 06/03/22 | 17:00 | Bordeaux vs Troyes | 2.29 | 3.48 | 2.93 |
| 10. 06/03/22 | 17:00 | Bologna vs Torino | 2.60 | 3.29 | 2.69 |
| 11. 06/03/22 | 19:00 | Antalyaspor vs Sivasspor | 2.57 | 3.21 | 2.67 |
| 12. 06/03/22 | 19:00 | Fenerbahce vs Trabzonspor | 2.38 | 3.21 | 2.91 |
| 13. 06/03/22 | 19:30 | FC Koln vs Hoffenheim | 2.70 | 3.40 | 2.50 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 02/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1116 | Boluspor vs Tuzlaspor | 2.07 | 3.32 | 3.17 |
| 16:00 | 1410 | FC Alania Vladikavkaz vs Arsenal Tula | 2.30 | 3.27 | 2.79 |
| 16:00 | 3932 | Tanzania Prisons vs Mtibwa Sugar | 4.00 | 2.90 | 2.14 |
| 16:30 | 4317 | Tobol Kostanay vs Kairat Almaty | 2.09 | 3.04 | 3.42 |
| 16:50 | 2968 | Lekhwiya SC vs Umm-Salal SC | 1.16 | 6.79 | 10.67 |
| 17:00 | 3435 | NK Radomlje vs Tabor Sezana | 2.23 | 3.28 | 2.89 |
| 17:00 | 4837 | Sivasspor vs Fatih Karagumruk | 2.11 | 3.32 | 3.08 |
| 19:00 | 5469 | Nomme Kalju vs Kuressaare | 1.28 | 5.21 | 7.72 |
| 19:30 | 3183 | Hajduk Split vs HNK Gorica | 1.17 | 5.97 | 13.48 |
| 19:30 | 5720 | NK Mura vs NK Celje | 1.98 | 3.46 | 3.27 |
| 20:00 | 1371 | Olympiakos vs Asteras Tripolis | 1.34 | 4.53 | 9.26 |
| 20:00 | 1537 | Paeek vs AEK Larnaca | 7.51 | 4.24 | 1.37 |
| 20:00 | 2513 | FC Sion vs Lausanne-Sport | 1.91 | 3.50 | 3.75 |
| 20:00 | 3372 | Spartak Moscow vs Urozhay Krasnodar | 1.17 | 5.96 | 12.50 |
| 20:00 | 3376 | Sparta Prague vs Baumit Jablonec | 1.47 | 4.06 | 5.80 |
| 20:00 | 5648 | ES Setif vs JS Kabylie | 1.75 | 2.85 | 5.61 |
| 20:30 | 1532 | Monza vs Parma | 2.11 | 3.14 | 3.48 |
| 20:30 | 2938 | Besiktas vs Kayserispor | 1.44 | 4.14 | 6.17 |
| 20:30 | 3416 | Lecce vs Ascoli | 1.65 | 3.62 | 5.09 |
| 20:30 | 4060 | Hamburger SV vs Karlsruher SC | 1.68 | 4.01 | 4.61 |
| 20:30 | 4888 | Tammeka Tartu vs Flora Tallinn | 16.35 | 6.35 | 1.13 |
| 20:30 | 5061 | Amazulu vs Stellenbosch | 2.13 | 2.80 | 3.93 |
| 20:30 | 5546 | Hannover vs RB Leipzig | 6.81 | 5.01 | 1.40 |
| 20:30 | 5684 | Frosinone vs Cosenza | 1.41 | 4.32 | 7.07 |
| 20:55 | 3880 | Voluntari vs CFR Cluj | 4.01 | 3.23 | 1.92 |
| 21:00 | 3486 | Zamalek vs Coca Cola | 1.56 | 3.65 | 6.31 |
| 21:00 | 3914 | Hapoel Haifa vs Bnei Yehuda | 1.57 | 3.67 | 5.21 |
| 21:00 | 4215 | Hallescher vs Viktoria Berlin | 1.78 | 3.63 | 4.13 |
| 21:30 | 5869 | AEK Athens vs PAOK | 2.32 | 3.21 | 3.01 |
| 22:00 | 2972 | Bekescsabai Elore vs Ujpest FC | 4.83 | 4.35 | 1.51 |
| 22:15 | 2848 | Luton Town vs Chelsea | 7.67 | 4.82 | 1.36 |
| 22:30 | 2101 | LASK Linz vs RB Salzburg | 2.51 | 3.67 | 2.33 |
| 22:30 | 3565 | FC Luzern vs FC Zurich | 3.05 | 3.45 | 2.19 |
| 22:30 | 3781 | Southampton vs West Ham | 2.29 | 3.34 | 2.95 |
| 22:30 | 5610 | Kilmarnock vs Raith Rovers | 1.78 | 3.24 | 4.35 |
| 22:45 | 1624 | Legia Warszawa vs Gornik Leczna | 1.41 | 4.33 | 6.16 |
| 22:45 | 1911 | St Johnstone vs Rangers | 10.82 | 5.31 | 1.26 |
| 22:45 | 2562 | VfL Bochum vs SC Freiburg | 3.20 | 3.35 | 2.23 |
| 22:45 | 2699 | Celtic vs St Mirren | 1.11 | 8.08 | 18.73 |
| 22:45 | 2915 | Livingston vs Dundee Utd | 2.15 | 3.10 | 3.49 |
| 22:45 | 3374 | Motherwell vs Ross County | 2.24 | 3.16 | 3.21 |
| 22:45 | 3659 | Hearts vs Aberdeen | 2.16 | 3.15 | 3.39 |
| 22:45 | 4077 | Dundee FC vs Hibernian | 3.45 | 3.25 | 2.10 |
| 22:45 | 4358 | Brugge vs KAA Gent | 2.23 | 3.32 | 2.98 |
| 23:00 | 1446 | Mallorca vs Real Sociedad | 3.35 | 3.20 | 2.22 |
| 23:00 | 4303 | Fiorentina vs Juventus | 2.80 | 3.19 | 2.48 |
| 23:15 | 3789 | Liverpool vs Norwich City | 1.17 | 6.90 | 12.82 |
| 23:15 | 4250 | Nantes vs Monaco | 3.49 | 3.24 | 2.08 |
| 23:30 | 5465 | Valencia vs Athletic Bilbao | 2.70 | 3.05 | 2.65 |
| 23:45 | 5190 | Sporting Lisbon vs Porto | 2.39 | 3.03 | 2.84 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# BIASHARA YAZITAKA 3 ZA SIMBA



**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Vivier Bahati, amesema amejiandaa vema kuwakabili Simba katika mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaopigwa Ijumaa wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Tayari Biashara United imewasili jijini Dar es Salaam kwa ajili ya mchezo huo ambao utakuwa wa kwanza kwa timu hiyo katika mzunguko huu wa pili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Vivier alisema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya kukabiliana na Simba kuhakikisha wanapambana kutafuta pointi muhimu.

Alisema anatarajia mchezo huo utakuwa wa ushindani mkubwa na mgumu kwa sababu Simba na wao wanahitaji pointi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kuwania ubingwa.

"Hii mechi itakuwa ngumu sana kwa sababu tunacheza na Simba ambayo imetoka kupoteza mchezo wao wa kimataifa na wanapambana kutafuga pointi muhimu ili kujiweka katika nafasi ya kutetea ubingwa," alisema Vivier.

Alisema amefanyia kazi mapungufu ya kikosi chake, umakini wa safu ya ushambuliaji na kuongeza mbinu kwa mabeki wake ili kupoteza katika mchezo huo.

Kocha huyo alisema wanahitaji kuanza vizuri mzunguko wa pili kwa kutafuta pointi dhidi ya wenyeji wao hao kama ilivyokuwa katika mchezo wa duru la kwanza.

Aidha, alisema wachezaji wote wanaendelea vizuri na hakuna mchezaji yeyote ambaye ni majeruhi na kwamba wamesafiri na kikosi cha wachezaji 24 ambao anaamini watatoa ushindani kwenye michezo yao yote miwili watakayoicheza wakiwa Dar es Salaam.

Baada ya mechi hiyo, Biashara United itakuwa mgeni wa Ruvu Shooting iliyoko juu yao (nafasi ya 12) kwa pointi moja zaidi, lakini yenyewe ikicheza mechi 16 hadi sasa.



# Ushindi waipa kiburi KMC

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuitwanga Polisi Tanzania mabao 3-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara Jumamosi iliyopita, KMC imeanza tambo ikidai imeiandalia Coastal Union kipigo kizito kwenye mechi itakayochezwa Jumatatu ijayo, Machi 7, Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala, amesema mpaka sasa hawajajua kama mechi hiyo itachezwa kwenye Uwanja wa Uhuru au Azam Complex, lakini kwa vyovyote vile itakavyokuwa watacheza Dar es Salaam dhidi ya Coastal na wanatarajia kupata ushindi mnono.

"Kwanza tunashukuru kwa matokeo dhidi ya Polisi Tanzania kwa sababu hatukuwahi kuwa na historia ya kuifunga timu hiyo, lakini safari hii tumewafunga, hii inaonyesha kuwa kikosi chetu kimezidi kuimarika.

"Kwa sasa tunajiandaa na mechi ya Machi 7, tumepangwa kucheza dhidi ya Coastal Union saa 10:00 kwenye Uwanja wa Uhuru, lakini huenda pia mechi hiyo ikachezwa Azam Complex, Chamazi, mara nyingi imekuwa hivyo, kwa hiyo mpaka sasa bado hatujua, ila tumejiandaa kupata ushindi mnono," alisema Mwagala.

Ushindi ilioupata KMC umewapeleka hadi nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa imejikusanyia jumla ya pointi 22 kwa michezo 16 iliyocheza, huku Polisi Tanzania ikisalia kwenye nafasi ya tisa kwa pointi 19, ikicheza michezo 16 pia.

# Michezo

Jumatano Machi 2, 2022
Nipashe



Laporta: Dembele atabaki Barca UKURASA 21

WEEEH!...



Mshambuliaji wa Yanga, Said Ntibazonkiza, katika harakati za kutaka kufunga, akimruka beki wa Kagera Sugar, Dickson Mhilu kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa mwishoni mwa wiki na wenyeji hao kushinda 3-0. **MPIGAPICHA WETU**

## Lwanga kukinukisha Simba, Biashara Utd

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Simba kimerejea jana kikitokea Morocco baada ya kuondoka nchini kwa zaidi ya wiki mbili sasa kwenda kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa, Kombe la Shirikisho Afrika na leo kitaingia kambini tayari kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Biashara United.

Simba ambayo imetoka kuvuna pointi moja katika michezo miwili ya ugenini ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya USGN ya Niger kisha kuhitimisha kwa kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya RS Berkane ya Morocco, inatarajia kuwapa nafasi wachezaji wake waliorejea kutoka chumba cha majeruhi katika mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumatatu ijayo.

Majeruhi wa muda mrefu ambao wanaelezwa kuwa fiti kwa sasa ni pamoja na kiungo mkabaji Taddeo Lwanga, ambaye alimekuwa akifanya mazoezi ya pamoja na kikosi cha kwanza kwa muda sasa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na uongozi wa klabu hiyo, baada ya kusajili jana, wachezaji wamepewa mapumziko na leo jioni watawasili kambini kuanza maandalizi ya mchezo dhidi ya Biashara United.

"Katika mchezo huo tunatarajia kuwapa nafasi wachezaji wengi ambao walikuwa majeruhi na sasa wapo fiti baada ya kupona," ilieleza taarifa hiyo.

# Hesabu ubingwa zamtesa Nabi

**Na Saada Akida**

### ●●● Atoa darasa kwa wachezaji wakiifuata Geita Gold Kirumba Ijumaa, Fei Toto na Job...

LICHA ya kuongoza msimamo wa Ligi Kuu Bara kwa pointi 11 zaidi ya mpinzani wao wa karibu, Simba, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi amesema hesabu za ubingwa bado ni ngumu na kwamba wanahitaji kuendelea kufanya maandalizi mazuri katika kila mchezo bila kujali aina ya mpinzani wanayekutana naye.

**Yanga inatarajia kuifuata Geita Gold FC Ijumaa wiki hii katika mechi itakayopigwa Jumapili katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, huo ukiwa ni mchezo wa pili kwao katika mzunguko huu wa pili wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 msimu huu.**

alisema mara nyingi anapokuwa kambini anazungumza na wachezaji wake kujituma na kujitoa katika mechi zilizopo mbele yao bila kujali aina ya mpinzani wanayekutana naye.

Alisema mzunguko wa pili wanatakiwa kuwa makini kuhakikisha wanapata pointi katika kila mechi bila kuangalia wanacheza na aina gani ya timu kwenye ligi hiyo.

"Hakuna mechi iliyokuwa rahisi, mzunguko huu, kila timu inahitaji kupambana kutafuta pointi, kuna wanaoshuka kujiweka katika nafasi nzuri na sisi tunahitaji kuendelea kujiimarisha kubaki katika nafasi tuliyopo sasa," alisema Nabi.

Alisema hawana muda wa kupoteza, Geita Gold FC ni wazuri, wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanapata pointi muhimu katika mchezo huo.

Wakati huo huo, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, amesema kikosi chao kinatarajia kuondoka Ijumaa kuelekea Mwanza tayari kuwavaa Geita Gold FC.

Alisema maandalizi yako vizuri hawana majeruhi mapya huku Kibwana Shomari, Abdallah Ninja, Crispin Ngushi tayari wameanza program ya mazoezi.

"Dickson Job na Feisal Salum 'Fei Toto' wamerejea uwanjani kwa kuwa tayari wamemaliza adhabu zao. Job amemaliza adhabu yake ya kufungiwa mechi tatu na Fei Toto adhabu ya kadi tatu za njano imeisha," alisema Bumbuli.

Alisema nyota hao watakuwa katika msafara wa kikosi kinachokwenda Mwanza Ijumaa kuivaa Geita Gold FC .

"Tunawasisitiza kwamba popote pale Yanga inapocheza inaenda kutafuta matokeo, CCM Kirumba ni nyumbani, tuna historia nako kwa kupata matokeo mazuri, tumejipanga mapema kwa sababu tulijua safari ya huko mapema sana," alisema Bumbuli.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >